Yesu Hutimiza Miadi Yake Yote

Tuendelee kusimama kwa dakika moja, na tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi. Na sasa wakati vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu, si—sijui, huu ukiwa ndio usiku ambao tumetenga sasa, kwa—kwa ajili ya usiku wa wokovu, kwa ajili ya kumjia Kristo na kumpokea Roho Mtakatifu, sijui ni wangapi walio na haja, na wangetaka kusema hili, "Bwana Mungu, nikumbuke. Ninataka kuwa sawa, Nawe, sasa"? Mwaweza kuinua mikono yenu juu? Bwana awabariki.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru sana kwa ajili ya Uwepo Wako, na kwa ajili ya watu wenye moyo mwaminifu ambao kweli wanaamini ya—ya kwamba Wewe unakuja, nao—nao hawana budi kujiandaa kwa ajili ya tukio hili kuu ambalo ulimwengu mzima umelingojea, maelfu haya yote ya miaka. Nasi tunaishi tu, tuseme, tukiangalia majira na historia zikiisha, nao Umilele ukianza kuingia. Nasi tunaona haya yakitukia, kwa hiyo mioyo yetu imepashwa moto kiajabu. Basi tunaomba, Baba, kwamba utaichunguza mioyo yetu usiku wa leo na kutujaribu. Na kukiwako na dhambi yoyote ndani yetu, Bwana, uiondoe. Tumeona juma hili, katika Uwepo Wako mkuu, wakati tukikutazama Wewe juu ya hili, miongoni mwa kusanyiko hili, ukishuka moja kwa moja na kuyachimbua mawazo yenyewe ya moyo, na kutufunulia, kutwambia mambo haya. Sasa, usiku wa leo, Bwana, tunataka mioyo yetu iwe mikweli na sawa na Wewe. Tunaomba ya kwamba utabariki.

3 Hapa jukwaani, ama mimbarani, limewekwa kasha la leso, vifurushi vidogo vinavyowaendea wahitaji. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, wa—wakati vinapotumwa kutoka mahali hapa, ambapo maombi yamefanywa, na imani ya kumwamini Mungu, kwamba—kwamba kila leso hapa, na kila kitambaa kidogo na kifurushi kinachomgusa mgonjwa, jalia waponywe. Kwa sababu, wasikilizaji hawa na sisi, pamoja, tunaomba kwa moyo mmoja kwamba utawaponya, Baba. Ni kumbukumbu ambayo tumeomba. Wewe ulisema, "Ombeni nanyi mtapata. Na mwombapo, aminini kwamba mnapata mnachoomba." Ninaamini, Bwana. Sote tunaamini. Na imeombwa. Sasa na itimizwe kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

4 Vema, hakika ni vema kurudi kwenye—kwenye ukumbi huu tena usiku wa leo, na chini ya matarajio makubwa kwamba

Bwana atatutembelea usiku wa leo, kwa kuwa tumeutenga usiku huu, kutoka kwenye kuwaombea wagonjwa, ili kuninii . . . kutafuta wokovu wa nafsi zetu. Kila mmoja wetu anapaswa kuyaweka maisha yetu wakfu upya tena. Pia juma hili tumeuona Uwepo wa Yesu Kristo, Maandiko yaliyothibitishwa, Yeye papa hapa miongoni mwetu, tukitazama yale aliyofanya. Mambo yale yale aliyofanya duniani wakati alipokuwa hapa hapo awali, anayafanya vivyo hivyo tu. Sasa, kama tukiona kwenye huduma wakati ikipanda, ni kama tu tunakua ili kuingia kwenye siku kamilifu, kanisa kamilifu. Tulianza . . . Kama tu—kama tulivyokuwa tukisema asubuhi ya leo.

5 Katika ushirika wetu mdogo mzuri, asubuhi ya leo, hakika tulikuwa na wakati wa ajabu sana kwenye kiamshakinywa hicho. Ninawashukuru ndugu hao kwa ajili ya ushirikiano wao mwema. Niliweza kupeana mikono na wengi wao, watu hawa wazuri wanaoudhamini mkutano huu, kutuleta humu. Kuninii . . . Inaonyesha ya kwamba wanawajali watu wao. Hao ni wachungaji, na wanawajali kondoo wao. Hivyo basi nina—nina shukrani sana ya kwamba baadhi ya hawa . . . Kila mchungaji ana shauku ya kuwapa kondoo wake vitamini. Nazo hizi ni vitamini za kiroho, tuseme, ambazo—ambazo huwasaidia kondoo kukua wakapata imani hodari katika Mungu wetu. Na kwa hiyo na—nawathamini watu kama hao.

6 Na sasa, tukizungumza asubuhi ya leo kwenye wazo la kukua kwa Kanisa, mnaona, likija kama Mbegu ardhini. Nayo Mbegu hiyo, inapopandwa, inakua kutoka utukufu hata utukufu. Nayo inakua, baada ya kitambo kidogo, inachanua, kisha inarudi kwenye mbegu. Hiyo ni kama Mbegu asili iliyopandwa. Ndivyo Kanisa limekuwa. Wakati wa kanisa ulianza, katika siku hizi za mwisho . . .

7 Baada ya nyakati za giza, ilianza na Martin Luther, katika yale matengenezo, akihubiri kuhesabiwa haki kwa imani. Baada ya wakati wake, basi wakaliundia kanisa dhehebu, likafa.

8 Kisha, mle ndani, akaja Zwingli, baada ya Luther. Naye Zwingli hata hakuamini katika uzao wa bikira. Alienda huko Uswizi. Wangali hawaamini, katika fundisho la Zwingli, hawaamini kwamba Yesu alizaliwa na bikira. Walisema alikuwa mwana wa Yusufu, *aitwaye* Mwana wa Mungu.

9 Lakini hiyo inaoandoa nguzo yote chini ya, msingi wote wa Ukristo. Yeye alizaliwa na bikira, la sivyo Yeye ni mwanadamu tu kama wewe ama mimi. Alikuwa ni Mwana wa Mungu.

Halafu, baada ya hao, akaja Calvin, na kuendelea na kuendelea.

10 Hatimaye, kanisa lilifikia kiwango ambacho, ililibidi kuwa na matengenezo mengine. Ndipo Mungu akamtuma John Wesley na ujumbe wa utakaso, usafi wa roho. Halafu yeye na Whitefield, na wengi wao wakaingia kwenye matengenezo hayo makuu,

na Asbury. Wakaja Marekani. Basi uamsho huo mkuu uliokoa Uingereza na ulimwengu, wakati huo.

11 Walifanya nini? Baada ya hao waanzilishi wote kufa, walianza kuunda madhehebu chini ya fundisho lao, na, muda si muda wajua, wakaunda dhehebu. Halafu wakatokea wengine waliotengana na hao, kama vile Alexander Campbell, John Smith, na kanisa la Kibaptisti, na kadhalika. Halafu Nazarayo, Pilgrim Holiness, na wengine wakatokea.

12 Ndipo yakaja yale matengenezo makuu tena, Pentekoste, wakitoka kwenye madhehebu hayo, wakiwa na kurudishwa kwa karama; kunena kwa lugha, uponyaji wa Kiungu. Miujiza mikuu na ishara zikatokea. Hilo liliendelea kwa muda mrefu. Imekuwa ni miaka hamsini, yapata miaka hamsini—themanini sasa, tangu Roho Mtakatifu alipoanza kushuka kwenye ile Barabara ya kale ya Azusa huko California. Hapa Marekani, ambako alianza kushuka, ukatokea wakati mzuri sana.

13 Basi, Pentekoste ilifanya nini? Moja lilijiundia dhehebu. Moja likasema, "Yeye yuaja juu ya farasi mweupe"; lingine, "Juu ya wingu jeupe." Nao hao wakaenda, katika madhehebu, na kutengana, wakivunja udugu wao miongoni mwa watu.

14 Na kama tu Israeli. Israeli hawakujua kabisa kwamba walipokuwa wakipiga makelele ya ushindi ufukoni mwa mto, walikuwa tu umbali wa safari ya siku nne, yapata maili arobaini, kutoka kwenye nchi ya ahadi. Hawakutambua walikuwa miaka arobaini, ingewachukua. Lakini ilikuwa ni nini? Neema ilikuwa imewapa nabii, Nguzo ya Moto, mwana-kondoo aliyetolewa kafara, ukombozi. Na hata hivyo bado walitaka torati. Wanataka kitu ambacho wangeweza kupata kitu cha kufanya mle. Wanataka kuingiza mikono yao mle. Hilo lilikuwa ndilo kosa la kijinga sana walilopata kufanya, katika Kutoka 19, hapo Israeli ilipoikataa neema ikakubali torati.

15 Halafu walifanya nini? Yeye aliwaacha tu wakae mle nyikani kwa muda wa miaka arobaini. Wakapanda mashamba ya mizabibu, na wakala tunda, na wakaoa wake, na kuwalea watoto, mpaka kizazi hicho cha kale kikafa chote na kizazi kingine kikaja. Miaka arobaini baadaye, wala hawakuwa umbali wa saa arobaini, bali iliwabidi kungojea muda wa miaka arobaini kabla hawajavuka. Ndipo kiongozi mpya akatokea, Yoshua, ndipo wakaingia nchini, wakiwa na kundi jipya.

16 Sasa, nafikiri ni mfano mzuri sana hapa, tunaouona. Zamani za kale, wakati baba zetu katika Pentekoste, walipoinuka. Walikuwa na ile Halmashauri Kuu ya kale, kutoka hapo ikaundwa Assemblies of God. Kutokana na hiyo ikaja UPC, halafu United, na kadhalika, mpaka wakapata dhehebu baada ya dhehebu, wakizozana na kushambuliana. Mungu aliwaacha tu waketi papo hapo, waoe wake, wakuze watoto, waseme kwa lugha, wapige makelele katika Roho. Lakini sasa kuna kundi

jipya ambalo limeinuka. Walikuwa tu umbali wa siku chache kutoka kwenye nchi ya ahadi. Baraka hizi zote walizokuwa nazo zilikuwa ni sawa. Lakini, kumbukeni, nchi nzima ilikuwa ni mali yao. Sasa tunajiandaa kuingia katika Nchi ya Ahadi, kwa hiyo Bwana na atusaidie tunapoyaangalia mambo haya. Mnaona?

17 Kama tu vile piramidi. Mliona jinsi piramidi ilivyojengwa? Sio fundisho la piramidi sasa; piramidi tu.

18 Angalia juu ya noti yako ya dola moja. Muhuri wa Marekani ni huyo tai. Vema, kwa nini inasema hapo kwenye hiyo piramidi, "Muhuri Mkuu"? Kwa nini uwe mkuu hapa kuliko Marekani na—na muhuri wa Marekani; Muhuri Mkuu, lile jicho, likiangalia?

19 Nalo—nalo jiwe la kufunika linalowekwa juu ya piramidi, lilikuwa . . . lilikataliwa. Kamwe halikuwekwa juu ya piramidi, halijawekwa hata wa leo; lile Jiwe la Skonsi, wanadai. Lakini kamwe halikuwekwa, jiwe la kufunika. Kwa nini? Wakati Henoko na hao wengine, katika siku za mwanzoni, walipozijenga piramidi huko Misri, tunaona, na mle ndani, walijua ya kwamba jiwe la pembeni, jiwe la kufunika, lingekataliwa. Nayo piramidi hiyo imewekwa kikamilifu sana pamoja hata hawahitaji mota. Ilichongwa vizuri sana kiufundi mpaka jiwe moja linashikana na lingine, yanabanana sana, hata huwezi kuweka wembe kati yayo. Sasa, iliendelea tu kulundikana, na sasa imechongoka, huko juu, tayari kwa ajili ya jiwe la kufunika litakapokuja.

20 Hivyo ndivyo Mungu amelileta Kanisa Lake, kutoka kwenye kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na sasa huduma ya Roho ambaye Ndiye hulihuisha Neno. Huduma hiyo Kanisani itabidi ifanane na Yake kabisa.

21 Kama hivi tu, wakati kivuli changu hapa, cha mkono wangu . . . Kama sijawahi kuuona mkono wangu, nimeona kivuli, kwa namna fulani kinaninii . . . Kinafifia, kinapoenda mbali. Lakini kinapokaribia zaidi na zaidi, kivuli na cha halisi vinakuja pamoja, mpaka vyote viwili vinakuwa kitu kile kile.

22 Na hivyo ndivyo hasa wakati Kanisa na Neno havina budi kuwa kitu kimoja, kama vile Yesu na Mungu walivyokuwa mmoja, kabisa. Hao . . . Mungu ananinii, alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake. Na vivyo hivyo itabidi Kristo awe Kanisani, mtiwa mafuta wa Neno, apate kutimiza kila kitu. Na hilo ndilo Jiwe la Kufunika linalokuja juu ya wakati wa mwisho wa kanisa. Sio Laodikia, sasa. Ni kuitwa kutoka humo, Bibi-arusi kutoka kanisani, Kanisa kutoka katika kanisa, kwa maneno mengine, kama tu vile Yeye alivyoliita taifa kutoka kwenye taifa, huko Misri. Na sasa tunaishi katika siku hiyo, nasi tunashukuru kwa ajili ya mambo haya makuu ambayo tumekuwa tukiyaona.

23 Sasa, kesho alasiri, Bwana akipenda, itakuwa ni kumalizika kwa ibada hii, sehemu hii ya ibada. Nasi tutautenga huo kwa jumla kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa. Basi kila mtu

anayetaka kuombewa anaweza kuja na kuchukua kadi ya maombi, apate kupitia kwenye mstari wa maombi. Sasa, sababu ya sisi kusambaza kadi za maombi kwa hawa, ni kuwafanyiza mstari. Halafu basi, usipowafanyiza, wanaendelea kupitapita huku, huku, huku, unaona. Hao, kwa hiyo unaninii... Tunawapa kadi ya maombi. Unapata kadi ya maombi, kisha unaingia mstarini. Nawe utaona na kuamini, utauona utukufu wa Mungu ukitukia. Litakuwa jambo kuu.

24 Na sasa tunawashukuru kwa yote mliyofanya, na kwa makaribisho makuu ambayo tumekuwa nayo miongoni mwa ndugu hawa wahudumu na kadhalika.

25 Sasa, kesho ni Jumapili, nayo makanisa haya yatakuwa yamefunguliwa. Hakutakuwako na ibada hapa kesho asubuhi. Kutakuwako na shule ya Jumapili. Nanyi wageni...Ninao marafiki humu ndani, mimi mwenyewe, wa—walio pamoja nasi kwenye kundi hili, na wengine ambao wametoka kwangu mjini, hapa wawe pamoja nasi.

26 Sasa, hawa ndio watu ambao wanaudhamini mkutano huu. Wanaamini mkutano wa namna hii. Kama ningaliishi hapa katika mji huu, ningekuwa mfuasi wa moja ya makanisa yao. Hakika ningekuwa, maana wanaamini jambo lile lile ninaloamini. Nami ningekuwa mfuasi wa moja ya makanisa yao, kama ningaliishi hapa.

27 Nanyi ambao mliyatoa maisha yenu kwa Kristo juma hili, wala hamna kanisa la nyumbani, mbona msishauriane nao? Wanaamini jambo lili hili, la sivyo wasingekuwa wameketi hapa wakiliwakilisha. Mnaona? Kwa hiyo sasa, ji—ji—jitafutieni moja zuri, moja ya makanisa haya mazuri, kesho, na mwende kwa hilo. Nina hakika watawatendea wema. Watawasaidia. Watawasidia kuamini. Na endapo hamjabatizwa, waulizeni. Endapo hamjampokea Roho Mtakatifu, waulizeni kuhusu hilo. Nao watawasidia moja kwa moja kumwendea Kristo, na kuwachunga kote kote safarini mpaka Yeye atakaporudi. Sasa, Bwana ambariki kila mmoja wenu.

28 Na sasa, mwajua, wanasema, Wapresbiteri daima husimama na kuketi chini. Bali mimi si Mpresbiteri. Lakini ninaamini ya kwamba tunapolisoma Neno inatupasa kusimama, kwa kuwa ni heshima kwa Mungu, kusimama. Kama tu vile tunavyoipigia bendera saluti, ama kutoa heshima yetu, ama chochote kile.

29 Basi sasa, kwa ajili ya usiku wa leo, nimechagua Maandiko ya kusoma hapa, kutoka katika Kitabu cha Luka Mtakatifu, mlango wa 7, kuanzia kifungu cha 36.

30 Basi sasa, juma zima nimekuwa nikilishughulikia wa—wazo lililonijia, barabarani wakati nikielekea huku, juu ya, “Kufunuliwa kwa Mungu mkuu.” Lakini nilipomaliza, kuyaangalia Maandiko yangu na kadhalika, nilikuwa na karibu kurasa ishirini. Kwa hiyo kamwe nisingeweza kuumaliza

huo, kwa muda wowote hapa. Kwa hiyo nikawazia ingenibidi kulibadilisha usiku wa leo, kwa hiyo nimelibadilisha.

31 Ninaamini ni mapenzi ya Bwana kwamba niseme mambo haya. Sasa, katika mlango wa 7 wa Luka Mtakatifu, na kifungu cha 36.

> . . .*mmoja katika Mafarisayo alimwalika ale chakula kwake; akaingia katika nyumba yake yule Farisayo, akaketi chakulani.*
>
> *Na tazama, mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi, alipopata habari ya kuwa Yesu ameketi chakulani katika nyumba ya yule Farisayo, alileta chupa ya marimari yenye marhamu.*
>
> *Akasimama nyuma karibu na miguu yake, akilia, akaanza kudondoshea miguu machozi yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, akiibusu miguu yake na kuipaka ile marhamu.*
>
> *Basi, yule Farisayo aliyemwalika alipoona vile, alisema moyoni mwake,* (kumbukeni, sio kwa sauti kuu), *moyoni mwake. Akisema*, Kama mtu huyu. . .alikuwa *nabii,* angetambua *mwanamke huyu* aliyemgusa. . .*ni nani, naye ni wa namna gani, ya kwamba ni mwenye dhambi.*
>
> *Yesu* alijibu na *kamwambia, Simoni, nina neno nitakalo kukuambia. Naye* akasema, *Mwalimu, nena.*
>
> *Akasema, Mtu mmoja mkopeshaji alikuwa na wadeni wawili;* nao walimwia. . .*mmoja amwia dinari mia tano, na wa pili hamsini.*
>
> *Nao walipokuwa hawana cha kumlipa, aliwasamehe wote wawili. Katika hao wawili ni nani atakayempenda zaidi?*
>
> *Simoni akajibu akasema, Nadhani ni yule ambaye alimsamehe nyingi. Akasema, Umeamua haki.*
>
> *Akamgeukia yule mwanamke, akamwambia Simoni, Wamwona mwanamke huyu? Niliingia nyumbani* kwako, hukunipa *maji kwa miguu yangu; bali huyu amenidondoshea machozi miguu yangu, na amenipangusa kwa nywele za kichwa chake.*
>
> *Wewe* hukunibusu*; lakini huyu tangu nilipoingia hajaacha kunibusu sana miguu yangu.*
>
> *Hukunipaka kichwa changu mafuta; bali huyu amenipaka miguu yangu marhamu.*
>
> *Kwa ajili ya hayo namwambia,. . .nakwambia, Amesahehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana; lakini asamehewaye kidogo, huyo hupenda kidogo.*

Kisha alimwambia mwanamke, Umesamehewa dhambi zako.

Ndipo wale walioketi chakulani pamoja naye wakaanza kusema mioyoni mwao, Ni nani huyu hata asamehe dhambi?

Akamwambia yule mwanamke, Imani yako imekuokoa, enenda zako kwa amani.

32 Na tuombe.

33 Bwana Yesu, hadithi hii ilitukia miaka mingi iliyopita. Lakini ni hadithi ya kweli, kwa kuwa imeandikwa katika kurasa za Biblia yetu, nasi tunajua ya kwamba ni ya kweli. Na sasa kamwe tusingejaribu kuonyesha hili tena usiku wa leo, ila tungependa utusaidie kuleta huu kama ujumbe usiku wa leo kwa watu, ili waweze kuona ya kwamba—ya kwamba ungali ni Bwana Yesu yeye yule. Nasi tunaomba baraka Zako juu yetu sote, kwa kuwa sisi ni watu wahitaji. Tunakuhitaji, Bwana.

34 Nasi tunaamini, usiku wa leo, ingawa tunaona Wewe unawafanya vipofu kuona, na viziwi kusikia, na viwete kutembea, na—na kwa taarifa za daktari tumekuona ukiwafufua watu watano katika wafu, nyakati mbalimbali, katika mataifa mbalimbali; lakini hata hivyo, Bwana, ninaamini, kitu kilicho kigonjwa kuliko vyote nikijuacho usiku wa leo ni mwili wa Kristo hapa duniani, kanisa. Ni mgonjwa kweli. Liponye usiku wa leo, Bwana. Sehemu hii inayoketi pamoja hapa, kundi hi—hili linalokaa hapa Ta—Tampa, kundi hili la watu wa kupendeza, Bwana, ponya kila jeraha usiku wa leo. Roho na atujalie hili, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa heshima Yake na kwa utukufu Wake, hapa katika jiji hili ambamo tunasafiri. Amina.

35 Mwaweza kuketi. Kama ningeweza kuliita sasa, kwa dakika chache tu . . . Na kujaribu nisininii, kila usiku . . .

36 Sina budi kuwaomba msamaha. Kwa kuwa mmekuwa wema sana, nanyi ni wasikilizaji walio rahisi sana kuhubiria, hata ni vigumu kujua pa kukomea. Na hiyo inamfanya mhudumu kujua ya kwamba mnakula, ama mnayapokea maneno ninayosema.

37 Nimekuja kwenu wakati nimekuwa . . . Nimechoka kuliko nilivyopata kuchoka, tangu sijui lini. Mnaona, sijapumzika tangu Krismasi.

Nikitoka hapa naenda moja kwa moja hadi Tucson, na kuanza tena.

38 Nitoke huko moja kwa moja, na kuenda British Columbia, kubatiza kabila lote la Wahindi ambalo nililiongoza kwa Kristo, lililokuwa ni la Kikatoliki, majira yaliyopita ya majani kupukutika, nilipokuwa kwenye ziara ya kuwinda. Nalo kundi hilo lote likaitoa mioyo yao kwa Kristo, kwa kuponywa kwa mama, mmoja wa hao akina mama. Huyo, madaktari,

hakuna mtu, angaliweza kumgusa. Alikuwa amelala, akifa. Nao wananitaka nirudi, mara barafu itakapoyeyuka. Mnaona, inafikia themanini na tano chini ya sufuri kule. Na kwa hiyo, hapo barafu itakapoyeyuka, ninawachukua, wote hao.

39 Kundi kubwa mno la wategaji na wawindaji, huku na huku kwenye Barabara Kuu ya Alaska, wote wanakutana na mimi, kubatizwa na kumkubali Kristo. Walimwona Bwana akionyesha ono la kitu fulani, ambapo dubu mmoja angekuwa, atakuwa na ratili ngapi, alikuwa ni wa aina gani, na mahali mnyama fulani atakuwa amekaa; jinsi, ni nani angekuwa pale, na kile watakuwa wamevaa, na yote kuhusu hayo. Na niliwaambia kabla halijatukia. Nao wakasema, "Hata hakuna vitu kama hivyo katika nchi hii." Nasi tukaenda moja kwa moja kwake. Lilitukia, neno kwa neno. Kumbukumbu hizo zimetundikwa chumbani mwangu leo hii. Mnaona? Walisema, "Tunataka kubatizwa pia." Watu wakali, lakini, mwajua, Yeye ana mbegu imekaa kila mahali.

40 Somo langu usiku wa leo ni: *Yesu Hutimiza Miadi Yake Yote*. Ninawatakeni mweke hilo niani mwenu tunapozungumza. Na si—sitazungumza kwa muda mrefu kupita kiasi. Nami nawatakeni mliwazie sasa. Kumbukeni, huna budi kukutana na Huyu aliyepo pamoja nasi usiku wa leo, siku moja.

41 Sasa, hapana budi ilikuwa ni karibu machweo, wakati mandhari yetu inapoanza usiku wa leo. Hapana budi ilikuwa karibu na machweo. Naye tarishi huyu alikuwa amekimbia siku nzima, labda siku mbili ama tatu. Alikuwa akijaribu kumpata. Alishuka akaenda, labda, karibu, kutoka Dani hadi Beersheba.

42 Kwa sababu, Yesu, katika huduma Yake, alikuwa akienda. "Anazungumza hapa," anafanya ishara na maajabu Yake, nao watu wote wangekutanika. Angeondoka, mahali pengine. "Sina budi kwenda katika mji mwingine."

43 Naye alikuwa amepitia wakati mgumu. Labda alikuwa ameenda huko Kapernaumu, nao wakasema, "Mbona, Yeye aliondoka hapa juma moja lililopita. Hatujui alienda wapi hasa, lakini alienda mahali pengine." Naye, loo, alikuwa amechoka. Nywele zake zilikuwa zimejaa jasho, miguu yake imejaa mavumbi na jasho, wakati akija kwenye umati ambapo Yesu alikuwa akizungumza.

44 Naye Yesu pia alikuwa amechoka. Alikuwa akizungumza siku nzima. Mdomo wake ulikuwa umekauka, kutokana na kuzungumza sana. Nayo mikono yake ikaanza kuonekana yatetemeka, na macho yake machovu, wakati jua lilipoanza kutua.

Naye alitaka kumwona Yesu. Alikuwa na ujumbe kwa ajili Yake.

45 Na sasa, Yesu alikuwa na watu kumi na wawili waliomzunguka, waliowazuia watu wasimkaribie, maana

wangemsukuma tu. Na kwa hiyo wakaninii . . . Ninalifanya hili kama mchezo wa kuigiza, kusudi kila mtu aweze kuushika. Na kwa hiyo tunaona kwamba, katika jambo hili, watu wa Yesu, hapana budi alikuwa amekuja . . . Hebu tuseme alimjia Filipo. Naye Filipo huenda alisema kitu kama hiki, "Bwana," ama, "Kijana, bila shaka tungetaka kukuacha umwone Bwana, lakini—lakini amechoka sana. Sisi, hatuna budi kumchunga, kwa sababu Yeye—Yeye huendelea tu mpaka karibu azimie. Nasi tumekuwa kwenye mikutano mingi sana na kadhalika, hivi majuzi, mpaka, nasikitika, siamini tungeweza kukuruhusu."

46 "Lakini," anasema, "Ni—nina waraka hapa, unaotoka kwa mtu mashuhuri sana katika mazingira ya kidini. Na ni mwaliko kwa Bwana wenu, ambao utakuwa ninii kuu—jambo kuu i—ikiwa ataenda. Nami sina budi kumwona. Kwa sababu, nimeagizwa, kwamba sharti nimpelekee waraka huu, na nihakikishe kwamba anaupata yeye."

47 Kwa hiyo, hatimaye, wakampeleka kwa Bwana Yesu. Basi alipokuwa akimwangalia, Bwana Yesu; labda akiondoka mahali pake (mimbara) ambapo alikuwa akizungumzia, ambapo wanafunzi na hao wengine walikuwa wamemwandalia azungumzie. Alipokuwa akiangalia, mbona, alimwangalia kijana huyo. Hapana shaka alimpenda.

48 Basi kijana huyo akamwambia. Akasema, "Mimi ni—nimetumwa, Bwana. Na kuna mtu mwenye cheo kikubwa sana huko kwenye mji fulani. Naye ni Farisayo, dini yenye msimamo mkali kuliko zote. Naye ana—anafanya cha—chakula cha mchana, wakati mzuri sana, dhifa. Naye anakutaka uje, uwe mgeni wa heshima. Naye ni . . . Wengi wangetaka kuhudhuria dhifa hii, bali amekuchagua Wewe. Nami nimejaribu kukutafuta siku tatu, kote nchini. Na bila shaka nilifurahi kufika hapa, Bwana. Nami nitakupa waraka huu, kutoka kwao, na kutoka kwake."

49 Basi akachukua waraka huo akausoma. Nasi tunaona ya kwamba Farisayo huyu alikuwa . . . alikuwa akifanya sherehe, na—na alikuwa amemwalika aje na awe mgeni wa heshima pamoja naye. Kwa hiyo, Yesu akisimama kwa dakika chache akimwangalia huyu kijana mwanamume.

50 Na hata hivyo ingawa alikuwa na shughuli nyingi sana, bali kamwe huwezi kumwalika pasipo Yeye kuja. Sijali hali ikoje, Yeye atakuja.

51 Akasema, "Mwambie bwana wa—wako kwamba nitakuwa hapo. Kwenye siku fulani hii, kwenye wakati fulani huu, nitakuwa hapo."

52 Hapana shaka huyo tarishi alitabasamu, ameridhika, kisha akageuka, akateremka mbio kilimani akampelekee bwana wake habari njema, kwamba alikuwa amefanikiwa kuupeleka ujumbe kwa Huyu aliyetaka.

53 Huyo tarishi alikuwa na shida gani? Ingewezekanaje? Je! alifahamu aliyofanya? Mara ya kwanza, labda, maishani mwake, ambapo alipata kusimama Mbele za Yesu, na hata hakuomba msamaha wa dhambi zake. Kamwe—kamwe hakuitumia fursa hiyo.

54 Loo, jinsi ilivyo vivyo hivyo na watu siku hizi. Mara nyingi wa—wanatambua kwamba wako Mbele Zake, wa—wala kamwe hawaombi msamaha.

55 Vema, hiyo, hu—huenda asipate fursa hiyo wakati mwingine, na huku alikosa kuitumia fursa yake ya mwisho ya kuomba msamaha. Angewezaje kufanya hivyo? Mvulana huyu angewezaje kuwa ameshikwa sana na kuuleta ujumbe huu kutoka kwa bwana wake, hata akashindwa, Mbele za Mwana wa Mungu, kuomba msamaha? Yote ilikuwa ni shughuli ya biashara.

56 Na, mwajua, hiyo ni kama vile watu siku hizi. Kanisa, Kristo, amekuwa ni shu—shu—shughuli ya biashara, ama shughuli ya jamii, kujiunga na kanisa na kupata msimamo mzuri kidogo wa kijamii kwa ajili ya biashara yako au kitu kingine. Unaonekana kuwa bora kidogo katika ujirani. Kweli si jambo la—la kuja na kutubu, kama impasavyo mwe—mwenye dhambi. Mara nyingi, kanisani, watu wanaletwa moja kwa moja Mbele za Kristo, nao wanaondoka na kufanya jambo la kijinga kama alilofanya huyu tarishi.

57 Loo, alipaswa kupiga magoti, na hapo alipotambua Yeye alikuwa Ndiye, naye aseme, "Bwana, nina ujumbe kwa ajili Yako, lakini, kwanza, ninaomba unisamehe." Huo ungekuwa ndio mtazamo mzuri. Ndipo kukiwako na shughuli nyingine ya kutekelezwa, hiyo ifanywe baadaye. Lakini, kwanza, aiweke nafsi yake sawa na Mungu.

58 Hiyo ndiyo sababu ninafikiri uponyaji mwingi hushindwa, ama wanaouita uponyaji. Kwa sababu, kwanza kabisa, watu hawako tayari kwa uponyaji. Hawatakiri makosa yao. Biblia ilisema, "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana." Nasi hatutaki kufanya hivyo. Kama tunaweza kuchukua uponyaji na kuendelea, na kurudi nyuma na kufanya yale tuliyokuwa tukifanya, wangekubali hilo. Lakini inapofikia kweli, kwanza, kuja na kujiweka sawa na Mungu, watu hawataki kufanya hivyo. Na hiyo ndiyo sababu inatupia—inatupia uponyaji wa Kiungu maji baridi. Unaona watu wengi sana wakiingia namna hiyo, na kutoka, wala hawaponi. Naye Mungu anajua yote kuhusu hayo.

59 Sasa, jamaa huyu alifanya jambo la kijinga kweli, tungewazia. Tungewazia, "Laiti ningeweza kupachukua mahali pake. Laiti ningalienda mbele ya Kiti Chake cha Enzi, na—na kupeleka ujumbe, jambo la kwanza ningalifanya . . . " Ungefanya nini, ungevutiwa na yale dhehebu lako lilikutuma kupeleleza?

Ama, ungekuwa ukiangalia huku na huku, uone jinsi Mbinguni kulivyopambwa? Ama, Mbele Zake, lingekuwa jambo la kwanza ungesema, "Bwana Mungu, nisamehe, mwenye dhambi"? Hilo lingekuwa ndilo jambo zuri la kufanya.

60 Sasa, wakati Yesu alipokuwa akimwangalia mvulana huyo, na wakati alipoondoka, huenda liliingia niani Mwake, "Kwa nini mvulana huyo hakufanya hivyo?" Ni kwa sababu hakutambua Huyo alikuwa ni nani.

61 Hebu niseme hili, sio kukufuru. Naomba niseme hili, sio kwa sababu ni mkutano huu, ama mkutano wowote. Lakini nafikiri hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Watu hawalitambui. Wanaona Maandiko yametambulishwa kikamilifu, bali hawatambui ni Nani. Wataona jambo fulani, nao waseme, "Loo, hilo lilikuwa ni zuri sana. Hilo lilikuwa ni sawa. Mimi—mimi. . ." Lakini huelewi ni kitu gani. Kama ulifahamu, kungekuwako na toba ikiendelea, kulia na kuomboleza. Jiji hili lingekuwa na uamsho mkubwa sana, hata nusu yenu mngefungiwa, kabla ya asubuhi, hiyo ni kweli, kama tukifahamu kwamba ni Nini. Nasi tunapita, mara nyingi, na kuikosa fursa, kwa kutokufahamu.

62 Sidhani mvulana huyo kweli alitambua. Alikuwa amelelewa miongoni mwa Farisayo huyu, ambaye alikuwa ni mtawala m—m—mkuu, kiongozi, ama—ama mtu wa dini. Naye alikuwa amelelewa pamoja naye, na—na—naye akachukua tu upande wake wa dini. Naye huyo Farisayo alikuwa—alikuwa amemcheka Yesu, na kumdhihaki, ama jambo fulani walilofanya, kama hao siku hiyo. Naye akalitupilia mbali tu; hiyo haikuwa kitu ila "ujumbe wa kawaida tu" aliopaswa kuupeleka. Aliketi tu pale. Naye alikuwa Mbele Zake, wala hakuna lingine kwake. Haikumaanisha chochote kwake. Bali kama alikuwa na ufahamu; kama mvulana huyo angeweza kufufuka kutoka kwa wafu leo hii, na kuketi katika mkutano huu juma hili, angalifanya jambo fulani kulihusu. Angekuwa na ushuhuda ambao ungetutikisa sisi sote. Bali hakufahamu.

63 Sasa, kwenye mandhari hii hapa, kuna kasoro fulani. Kamwe si ninii. . .Sio sawa; wakati Yesu akimwangalia mvulana huyo akiondoka, amechoka na ni mchovu. Lakini, mandhari yote, kuna kasoro fulani. Hao Mafarisayo walimchukia Yesu. Basi kwa nini wamwalike kama mgeni wa heshima wakati walimchukia? Huyo Farisayo alikuwa, kama ule msemo wa kale wa mcheza kamari, alikuwa ameficha mtego. Alikuwa ameficha kadi ya ujanja. Maana, walimchukia Yesu. Ninaamini Yesu alitambua hilo, papo hapo. Mnaona, watu hawana budi kuwa na vitu shirika.

64 Mama yangu, alikuwa na msemo fulani, "Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba." Huoni, huwaoni koho na hua wakila pamoja. Hao ni—hao ni. . .Mmoja ni mla mizoga. Naye

hua asingekula chakula cha mwewe, kwa kuwa hana nyongo yoyote. A—asingeweza kuimeng'enya.

65 Wala huwaoni waaminio na wasioamini pamoja, isipokuwa pawe na kusudi fulani kwa hilo. Kuna kasoro fu—fulani. Jamaa huyu alikuwa ana mtego uliofichwa. Alitaka kumnasa Yesu.

66 Sasa, ukichukua watu, kama vile ukichukua vijana, watoto matineja, hawapendi kuwa karibu na wazee, kwa sababu wao—wana mambo shirika. Vijana waliofunga ndoa, wana mambo shirika. Wazee, hawataki kuwa karibu na watoto sana. Wa—wana mambo shirika.

67 Unapomwona msichana mdogo akifuatana na bikizee wakati wote, sasa, kuna—kuna kasoro hapo. Kuna tofauti kubwa mno katika umri wao. Ama ni kipenzi cha bikizee, la sivyo bikizee ana kifurushi cha peremende mahali fulani. Mnaona? Hapo, kuna—kuna ujanja mahali fulani. Nina mjukuu, mimi mwenyewe, nami najua. Kuna ujanja mdogo mahali fulani. Mnaona? Basi ukimwona akikaa karibu na bikizee, bikizee ana ki—kifurushi cha peremende mahali fulani ama kitu kingine.

Kwa hiyo huyu Farisayo alikuwa na mpango wa siri.

68 Yote yalitukia kwenye mkutano wa wahudumu ambapo wote hukusanyika. Nao mjadala ulijadiliwa kumhusu Jamaa huyu anayejiita nabii. Nao hawakuamini alikuwa nabii. Kwa sababu, wasingeweza kumwona mtu, ambaye asingeambatana nao, katika mafundisho yao yote, ambaye angeweza kuwa nabii. Na kwa hiyo, kwenye mkutano huu wa wahudumu, walikuwa wameamua ya kwamba Yeye hakuwa nabii.

69 Basi maskini Farisayo huyu alikuwa akitaka kuwathibitishia, kwamba Yeye hakuwa nabii. Farisayo huyu alikuwa akitaka ku—ku—kulihakikisha, na kulionyesha kusanyiko, watu wote humo mjini, kwamba Yeye hakuwa nabii, kabla hajautembelea mji huo. Hakuwa amewahi kufika kwenye mji huo hapo awali. Kwa hiyo, kabla hajaja, yeye alitaka kumfichua. Loo, roho hiyo, ingali hai. Amfichue, afanye jambo fulani litakalouzuia mkutano ambao angekuwa nao kule.

70 Kwa hiyo tunaona kwamba yeye alisema, "Nitaandaa chakula cha mchana, nami nitamwalika kila mtu, na kumwalika kila mtu mjini, huku. Ndipo tutathibitisha kwamba yeye si nabii. Tutalithibitisha."

71 Kwa hiyo, huenda Farisayo aliwaza kwamba, kwa kufanya hivi, angeninii—angepata ninii kidogo. . . labda awe, baada ya kitambo kidogo, mmoja wa wazee wa kanisa, ama chochote kile. Angekuwa—angekuwa. . . Kweli angepata sifa kubwa kwenye kundi lake. Alitaka kumdhihaki, kwenye dhifa hiyo, Bwana Yesu, kuthibitisha ya kwamba hakuwa nabii, amwingize matatizoni mahali fulani. Ndipo angekuwa jamaa mkubwa miongoni mwao, awe mtu mashuhuri.

72 Sasa, tunaona ya kwamba tarishi huyo anarudi na kumwambia bwana wake, "Nimempata. Aliahidi. Naye atakuwa hapa, kwa sababu niliona tu jinsi alivyotenda, a—atakuwa hapa." Vema.

73 Sasa, Farisayo huyo alingojea wakati huu maalum. Nao walijua wakati unaofaa wa kufanya dhifa hii, wakati kila kitu kilipokuwa sawa kabisa. Labda tutawazia, katika mchezo wetu mdogo wa kuigiza usiku wa leo, kwamba—kwamba aliifanya wakati zabibu zilikuwa mbivu. Kama ulipata kuwa huko Palestina kwenye msimu wa zabibu, ama hata California, wakati hivyo vishada vikubwa mno vya mizabibu vinachuruzika, vimeiva, nchi nzima, bonde limejaa—limejaa ha—harufu hiyo inayonukia vizuri kutoka kwenye zabibu hizo. Yeye alijua wakati uliofaa kabisa kuiandaa. Kwa hiyo, akapanga wakati huo, kwenye siku fulani watafanya karamu hii.

74 Mpaka, hatimaye, wakati ukawadia, ambapo karamu hiyo ingefanywa. Ndipo akamwalika kila mtu aje, aliyeweza, aje huko, waheshimiwa wote, na mashirika yote, na kadhalika, na vilabu vyote vilivyokuwa mjini, ambavyo alikuwa mwanachama wake. Wote walikuwa wakija kwenye ikulu yake kuu, ya kupendeza. Ilikuwa huko juu, ikajitokeza kama eneo humo mjini. Basi wakati ukawadia wa kufanya jambo hili. Bila shaka, uga ulikuwa umetengenezwa vizuri, na meza zikapangwa, na chumba cha dhifa tayari.

75 Na ndipo, sasa, itambidi kushughulikia ninii . . . wageni wake, watakapokuja. Mwenyeji yeyote atafanya hivyo. Kwa hiyo ilimbidi kukodi watunza farasi, maana baadhi ya wenyeji wake wangeku- . . . ama baadhi ya wageni wake wangekuja kwa magari ya farasi, na wengine wamepanda nyumbu, wengine wakitembea. Kwa hiyo mtu yeyote anayefanya ni—ninii . . . aliye na dhifa, hana budi kujiandaa, kuwaburudisha wageni wake. Kwa hiyo Farisayo akaandaa kila kitu, na watumishi wake wote, na kuwafanya tayari, akawaonyesha watunza farasi mahali wangewapeleka farasi, na nyasi zote kavu na kadhalika zikawekwa tayari kwa ajili yao.

76 Halafu alikuwa na mtunza nyumba ya kukaribisha wageni, ama bawabu, aliyepaswa kuchukua mialiko, maana u—usingeweza kuja isipokuwa umealikwa. Na kuchukua mialiko hiyo, alikuwa ameyaandika majina yao, kila aliyepaswa kuwa pale. Nao walipokuja, waliyatambulisha majina yao, ndipo waliweza kuingia.

77 Halafu, hebu tuangalie kile, kile kilichowabidi kufanya, kwa kitambo kidogo. Nimekuwa huko mashariki, na labda wengi wenu mmekuwa huko na mkaangalia jinsi wanavyofanya. Ni—ni jambo la kuvutia kweli. Nanyi mnaona, basi, wakati kila kitu kimeshughulikiwa, basi wanapofika mlangoni, jambo la kwanza, ba—bawabu anawauliza majina yao. Nao

wanasema majina yao. Anaangalia kwenye orodha yake, na hili hapa jina hilo, basi analiweka alama. Halafu kile afanyacho, yeye huchukua fimbo yake, na kuiweka pembeni. Wa—wavulana wanawachukua farasi, kama anatembea . . . ama kama amepanda farasi, na kumweka zizini.

78 Sasa jambo lingine analofanya, anaingia sebuleni. Na humu kuna kundi la—la watu, wanaoitwa, watawadha-miguu, watumishi. Ndiyo kazi yenye mshahara mdogo sana iliyopo, ni ya mtumishi mtawadha-miguu.

79 Na kuwazia hilo, sisi tunaofikiri ati tu watu maarufu, huku Bwana wetu alijitambulisha, duniani, kama mtumishi mtawadha-miguu. Hivyo ndivyo alivyofanya hasa. Halafu tunafikiri sisi ni watu maarufu. Tutakimbia hapa shuleni na kupata elimu kidogo, na kuninii . . . na kujifunza kusema maneno makubwa machache. Kisha tunarudi na kuvaa su—suti, na kutoka hapa nje na tunataka kuitwa "daktari, kasisi," ama mtu fulani.

80 Nilikuwa huko juu kwenye jumba kubwa la makumbusho sio muda mrefu uliopita, nikiangalia baadhi ya makadirio ya mtu mwenye uzito wa ratili mia moja hamsini, kwamba alikuwa na kiasi gani cha kemikali mwilini mwake. Mnajua ana kiasi gani akimiminwa kabisa? Ana thamani ya senti themanini na nne. Halafu utaweka kofia ya dola kumi juu ya senti themanini na nne, na koti la manyoya la dola mia tano, na kuinua pua yako juu; kama ilinyesha, ingekuzamisha. Halafu unaendelea, ukishughulikia hizo senti themanini na nne, kweli, ukiwazia kwamba wewe ni maarufu. Wala hujali, inavyoonekana, kuhusu nafsi hiyo iliyo na thamani ya ulimwengu milioni kumi. Hiyo tofauti yake, ujinga, jinsi tunavyoweza kuwa!

81 Sasa, huyu mtumishi mtawadha-miguu, ilibidi aioshe miguu yao. Sasa, katika ninii . . . Uliposafiri Palestina, vazi la Kipalestina ni joho. Huning'inia chini. Halafu vazi la ndani linafikia chini ya goti la mguu, *hapa*, vazi la ndani. Na kwa kuwa wa—wanyama na wanadamu wanapitia njia moja, wanyama, hakika, wakipitia njiani, na—na—na wana—wanapotembea njia moja. Ba—basi mavumbi yangetokea ambapo wanyama walipitia, na kulikuwako na harufu mbaya mavumbini. Nayo yakaingia miguuni mwao wakati wakitokwa na jasho. Nayo miguu yao imevalishwa makubadhi. Na hizo zote zingejaa jasho, na—na kulowa, zinanata.

82 Halafu harufu hii mbaya ambapo wanyama walikuwa wamepita njiani, ingeninii . . . Vazi la Kipalestina, likifagia chini kama sketi, chini, lingeokota mavumbi haya. Nayo yangeingia *humu* chini, na kuingia miguuni mwao mwote na mi—mikononi mwao. Nao kweli walinuka kama njia hi—hiyo ambamo hao wanyama walikuwa. Kwa hiyo, kuingia kwenye nyumba kama zile hao Mafarisayo walikuwa nazo . . . Waliagizia huko Uajemi

na kununua hayo mazulia mazuri makubwa mno, na—na kadhalika. Mbona, usingejisikia kukaribishwa, kuja mbele ya mwenyeji, na—na—na huku unanuka vibaya sana namna hiyo. Kwa hiyo walikuwa na njia ya kushughulikia hilo. Walikuwa na mtumishi mtawadha-miguu, naye alikaa pale.

83 Na mara ukiingia, nalo jina lako lilikuwa limeandikwa. Wavulana waliwachukua farasi ama wanyama wako, na kuwapeleka nyuma wakawalishe, kundi moja la wavulana. Halafu bawabu akakutambua kwa ile chati aliyokuwa nayo mkononi mwake. Ndipo basi uko tayari kwa ajili ya mtumishi mtawadha-miguu.

84 Ndipo unaingia. Unainua mguu wako. Anatoa makubadhi, anaziweka mahali fulani, kusudi ajue mahali ulipo. Halafu upande huu mwingine, ana kiatu kidogo. Na baada ya kumaliza kuiosha miguu yako, kuiosha vizuri sana, mavumbi yote na kadhalika, kukufanya safi, ndipo anakuvalisha maskini kiatu hiki cha nguo kinachofunika.

85 Kama vile unavyoona kwenye ndege unapovuka, kwenda nchi za ng'ambo sasa, wanakupa hivyo usiku. Wakati unaponinii. . .Kama vile wanawake walivyo na vitu hivyo vidogo wanavyovaa wakati hawavai stokingi. Mimi huona mke wangu na binti yangu na wengine wanavyo. Wakati mwingine wananinii. . .Kidogo ni. . .Si—sijui wanavyoviita, lakini ni kama sehemu ya chini ya soksi, mwajua, na—nawe unaivaa mguuni mwako.

86 Ni kitu kama hicho, ila tu ni kirefu kiasi, kwa maana hutaki kuchukua makubadhi yako machafu na kutembea juu ya zulia hizo mle ndani. Kwa hiyo, basi, miguu yako inaoshwa. Ndipo huna budi, jambo lingine linalotukia, umevaa kijibuti hiki, nitakiita hivyo.

87 Na halafu jambo jingine linalotukia, kuna mtu anayesimama pale na taulo begani mwake, naye ana marhamu mikononi mwake. Na hiyo ni mafuta ya manukato. Sasa, miali ya moja kwa moja ya jua hilo la Palestina juu ya shingo lako, inakutia tu malengelenge. Na jambo lingine, hayo mavumbi unayookota, wakati mwingine huingia kwenye ndevu zao na kwenye nywele zao. Ndipo mtu huyu husimama hapa, basi, na marhamu. Naye anaishikilia, kwenye kopo hili dogo. Unaimwaga mkononi mwako na kuisugua usoni mwako, na shingoni mwako. Ndipo unachukua taulo hii na kujipangusa, na kuchana nywele zako. Sasa wakati mwingine. . .

88 Hii ni adimu sana, maana kweli inatoa ha—harufu nzuri sana. Wanaipata mara nyingi kutoka juu ya mlima kabisa, kwenye kichaka mwitu cha waridi. Mmeona waridi baada ya petali kuanguka. Ndipo linakuwa—linakuwa kidogo—kidogo kama, tofaa, juu yake. Na kutoka hapo, wanalipondaponda na kutoa manukato haya. Inasemekana ya kwamba Malkia wa

Sheba, alipomjia Sulemani, alileta manukato haya mazuri mengi sana, akampa Sulemani. Adimu sana; ni vigumu sana kwenda milimani.

89 Basi wanapoyapangusa haya, ndevu zao na shingoni mwao, kwa taulo hii, wanajinadhifisha, sasa wako tayari ku—kukutana na mwenyeji wao, kukutana na yule aliyewaalika. Mnaona? Wasingejisikia sawa, kuingia na mavumbi hayo yote. Hiyo ndiyo sababu ya kutawadhwa miguu. Mnaona? Wa—wa—walikuwa wananuka vibaya, na iliwabidi waoshwe miguu yao. Na kukanyaga zulia hizo nzuri kwa makubadhi yao makubwa mazito, wasingejisikia sawa. Wangejisikia kuaibika. Bali sasa miguu yake imeoshwa, na sasa amenadhifishwa kabisa. Ananukia kwa manukato aliyopakwa, kutoka kwa marhamu hii, kile wanachoita "kupaka vichwa vyao mafuta", na kuyasugulia usoni mwao, kisha kuipangusa kwa taulo. Sasa amekuwa safi.

90 Sasa, jambo lingine analofanya, anakutana na mwenyeji wake, yule aliyemwalika. Anajisikia kukutana naye. Sasa, asingejisikia kukutana naye, akiwa mchafu hivi, kwa hiyo amenadhifishwa kabisa na yuko tayari sasa.

91 Ndipo mwenyeji anakutana naye mlangoni, nao wana njia ya kipekee sana. Na ingali iko kwenye baadhi ya makanisa, kusalimiana kwa busu. Kwa hiyo wanauchukua mkono, wanaukunja *hivi*, wanakumbatiana, wanaume, wa—wamekumbatiana, namna *hii*, na kubusiana shingoni. Basi mwenyeji anapokubusu, umekaribishwa. Hilo ni busu la kukaribisha. Sasa, usingetaka mwenyeji wako akubusu u—ukiwa na maskini uchafu huo wote na kadhalika, kwa hiyo huna budi kuoshwa vizuri kabla hujakaribishwa kwa busu. Lakini, loo, mara unapokaribishwa kwa busu, wewe ni ndugu kamili. Hivyo tu. Ungeweza, leo hii, jambo pekee unaloweza kufanya, kama siku hizi, ungeingia nyumbani, na kujisikia nyumbani. Wewe ni mmoja wao. Amekukaribisha kwa busu.

92 Mnakumbuka Yuda akimbusu Yesu, mnaona, kinafiki? Mnaona? Kwa sababu, kama alimbusu, ilikuwa ni kumkaribisha. Lilikuwa ni busu la rafiki, sio midomoni, bali shingoni, waliwabusu shingoni.

93 Sasa, tunaona basi, kwamba ungeweza kuingia. Kama ungalitaka kwenda kwenye friji, jinsi ingekuwa siku hizi, na kujipatia sandiwichi kubwa mno, ukalale kitandani na kuila, jisikie tu nyumbani. "Karibu. Ingia." Hiyo ni, uko sawa sasa. Unajisikia tu kama mmoja wa familia sasa, kwa sababu uko ndani.

94 Sasa, unafanya haya yote, na kupakwa mafuta, na kunadhifishwa. Umekaribishwa kwa busu. Kisha unaingia, unapeana mikono, halafu, kwenye dhifa. Unakutana na rafiki zako. Mwenyeji tayari amekubusu, uingie, na kwa hiyo uko—uko huru sasa. Unajisikia tu kama wewe ni mmoja wao. Umealikwa.

Umeoshwa. Umekaribishwa kwa busu, na sasa wewe ni mmoja wao. Ingia ukafanye ushirika wako.

95 Sasa, kwenye wakati huu, ningewazia nyama choma ya kondoo huko nje kwenye mahali pa kubanikia nyama huko nyuma, ilikuwa ikinukia maeneo hayo yote, pamoja na zabibu hizo na kadhalika. Ungewazia maskini wamesimama kote kwenye uzio, wakitona mate. Hawakuwa wamekaribishwa ndani; ni watu mashuhuri pekee, kwenye hii. Kwa hiyo ka—karamu ilikuwa ikipamba moto. Kila kitu kinaendelea vizuri; kabisa, imepamba moto.

96 Sasa, ningewazia Farisayo na nanii wake, rafiki zake wote, wanagonganisha bilauri, mmoja kwa mwingine, wakiburudika na kinywaji kizuri cha afya, na mvinyo mzuri sana uliokuwako Palestina wakati huo. Kwa sababu, walikuwa ni matajiri, wangeweza kuigharamia. Nao, kila mtu, wanawake, wanawake wao waliopambwa kwa vito vya thamani, walikuwa pale pembeni, wakifanya ushirika wao, wameketi kwenye kochi na kadhalika, kama ilivyokuwa desturi siku hizo. Nao wanaume, wote wamesimama wakitakiana heri, na kuzungumza, naye kuhani, na marabii wote, na kila kitu, wakiwa na wakati mzuri sana. Nayo ka—ka—karamu ikiendelea vizuri sana.

97 Halafu Yesu, ingawa alikuwa na shughuli nyingi, na ratiba yake yenye shughuli nyingi, Yeye daima hutimiza miadi Yake. Unaweza ukategemea hilo. Yeye hutimiza miadi Yake.

98 Sasa hebu tuangalie chumbani tuone kinachoendelea. Ninaweza kumwona Farisayo pale akigonganisha bilauri yake na kusema, "Rabii, unajua nini?" Na yale mazungumzo makubwa yakiendelea, wafanya biashara wakizungumza juu ya biashara zao na kadhalika. Dhifa iko—dhifa imepamba moto sasa, karamu hii kubwa.

99 Lakini, angalieni, mtu ameketi akiegemea ukuta, hawamwoni, alikuwa ni Yesu. Alitimiza miadi Yake. Akaja. Daima Yeye hulitimiza Neno Lake. Ahadi Zake zote, Yeye huzitimiza. Lakini hebu mwangalieni. Ameketi pale, mchafu. Ninachukia kusema hivyo. Linaniua kulisema. Lakini, miguu Yake ilikuwa michafu. Hakuwa amepakwa mafuta. Hakuwa amekaribishwa kwa busu, ingawa alialikwa.

100 Hiyo ni kama baadhi ya miamsho yetu ya kisasa. Wafaransa wanamwita, "Jésus, Jésus mwenye miguu michafu." Mngeweza kuwazia hilo? Yeye alialikwa akaja. Naye huyo hapo, ameingia kwa njia fulani, na pasipo kutambulikana. Anaketi pale kama ua la ukutani. Yeye alikuwa mahali ambapo hakubaliki tu pale, kama alivyo, kwenye baadhi ya miamsho yetu ya kisasa, dhifa, inayodhaniwa ni mikutano ya kidini.

101 Alikuwa mahali pasipofaa. Hakuna aliyekuwa akimjali. Walikuwa wamejishughulisha sana na mambo mengine, ingawa alikuwa amealikwa. Lakini, hakukaribishwa wakati alipokuja.

102 Ilikuwaje kwa huyo mtumishi mtawadha-miguu? Alikosaje fursa hiyo? Laiti ningalikuwa na fursa yake. Loo, jamani! Kama ningalijua alikuwa akija, ningalikuwa nimesimama pale nikimgojea. Ni—ningekuwa tayari kwa jambo hilo. Alifanyaje hilo? Sasa, hebu tusimhukumu kupita kiasi, kwa maana huenda tukafanya jambo lile lile wala tusijue. Mnaona? Alimkosa. Loo, jamani!

103 Angalieni, Yeye huja leo tunapomwita, pia. Yeye huja miongoni mwetu. Sitaki kusema hili, bali sina budi kulisema. Na miongoni mwetu, anafahamika miongoni mwetu, ameketi pale mchafu vivyo hivyo, kwa watu hao, kama alivyokuwa wakati huo, hiyo ni kweli kabisa, wakimwita "watakatifu wanaojifingirisha" na chochote kile. Na hata hivyo tunalia tupate uamsho. Naye anakuja. Na wakati ajapo, tunamfanyia karibu jinsi walivyomfanyia wakati ule.

104 Mtu fulani akisimama katika Roho wa Mungu, aseme kwa sauti kuu "amina," ama apige makelele, ama kitu kingine kama hicho, ikitokea Yesu anapita pale. Mbona, ninii . . . Wanafukuzwa kanisani. Vema, wanafikiri hiyo ni aibu mbaya sana, kuliaibisha kanisa, kuwaaibisha watu. Wakati, ni Yesu Mwenyewe akipita.

105 Nasi tunaweza kumwona akija na kulitambulisha Neno Lake, na kufanya kama alivyofanya wakati huo, na siku hizi wanasema, "Ni kupiga ramli, kuwasiliana kimawazo, ama roho mchafu." Mbele ya watu, Yeye ni mchafu tu kama alivyokuwa ameketi pale: Yesu, Neno la Mungu. Nasi hatujali. Tuna shauku sana ya dhehebu letu au msimamo we—wetu wa kijamii. Tunaona aibu kuitwa kwa Jina Lake. Kweli tunamwonea aibu.

106 Walimwonea aibu kwa sababu alikuwa ni mchafu. Wageni hawakumjua. Nao walimwonea aibu kwa sababu ni mchafu.

107 Hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Wangali wanamwonea aibu, kwa kuwa wanalundika uchafu wote wawezao juu Yake, na kuliita "watakatifu wanaojifingirisha" na kila kitu wanachoweza kuwazia. Hakuna mtu anayefanya kitu juu yake. Huyo hapo ameketi, miguu michafu, ua la ukutani karamuni, ua la ukutani katika mkutano wa kidini. Amealikwa, tunamwomba aje kwa ajili ya uamsho. Anapokuja, tunamtendea kama walivyomtendea kule. Anakuja, na kujitambulisha Mwenyewe, bali hakuna mtu anayetaka uhusiano wowote Naye.

108 "Kama angefanya namna fulani ya vitimbi, ama—ama—ama afanye namna fulani ya mu—mwujiza." Kama alivyofanya mbele ya Pilato . . . Pilato, fursa yake pekee aliyopata kuwa nayo, naye alimwomba, alitaka kuona kitu fulani kikifanywa, alitaka, "Hebu tuone ishara." Alipaswa kutubu.

109 Hivyo ndivyo ulimwengu huu katili, unaoelekea kuzimu unavyopaswa kufanya usiku wa leo, ni kuzitubia dhambi zao. Hivyo ndivyo hawa wafuasi wa kanisa wanavyopaswa kufanya, kutubia kutokuamini kwao. Wamtetee. Ni yeye yule jana,

leo, na hata milele. Naye hujitambulisha Mwenyewe jinsi tu alivyojitambulisha wakati huo. Nao watu siku hizi wanachukua msimamo ule ule kama aliouchukua yule Farisayo, msimamo kama ule; wanamwacha aketi, baada ya kumwalika. Hata hivyo, hawamtaki. Wanafanya hivyo tu, kama, tabia. Yeye anajua hilo.

110 Tumemfanyia Yeye, siku hizi, kama tu vile walivyofanya wakati ule; badala ya kumwosha, kumwoshea aibu (Yake), badala ya kujaribu kusimama, tukisema, "Umekosea. Ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Ni yale aliyoahidi Yeye. Alisema angeimwaga Roho katika siku za mwisho. Tunaishi katika siku za mwisho." Badala ya hilo, kwa namna fulani tunaketi tu kitako kama walivyofanya. Tunaogopa kuchukua msimamo.

111 Vipi kama mmoja wao angalisimama na kusema, "Huyo ni Yesu wa Nazareti. Ninaamini Yeye ni nabii wa Mungu"? Mnajua ni kwa sababu gani hawakufanya hivyo? Kwa sababu hawakuamini Yeye alikuwa ni nabii.

112 Na wangali hawaamini, leo. Wanafikiri Yeye ni mwalimu. Wanafikiri Yeye ni dhehebu. Hawajui Yeye angali ni nabii. Hiyo ndiyo sababu ya kumwalika kule chini, wakiswali. Hilo ndilo analoswaliwa leo hii. Hakuna mtu aliye tayari kumtetea. Wanasema tu, "Vema, sina uhusiano wowote Naye. Mnaona? Mimi ni mfuasi wa kanisa. Wale pale wachungaji wangu, wote hao, wameketi huku. Mimi ni mtu mwema." Naye Yesu akiwa na miguu michafu; hakuna aliyejali. Biblia yenyewe . . .

113 Sasa tunaenda na kupeana mikono, tunaandika jina letu kwenye kitabu. Nao Wa—Wamethodisti, kama hawatutaki, tutayapeleka kwa Wabaptisti. Wakitufukuza, tutaenda kwa Wanazarayo. Wa Umoja wakitufukuza, tunaenda na wa Uwili. Wa Uwili wakitufukuza, tunaenda kwa wa Utatu. Si lazima tulivumilie lolote la hayo. Wote ni baridi. Ni vivyo hivyo tu. Sisi . . .

114 Na wakati Yesu ajapo, hata hatutambui. Hatujali. Hivyo ndivyo wanavyofanya. Na hata hivyo tunalia, "Njoo, Bwana Yesu. Njoo, Bwana Yesu." Naye anakuja. Nasi tunafanya nini? Jambo lile lile walilofanya. Mbona? Kama wakisema lolote, kulikubali, mtu mwingine hapa atawadhihaki. Basi wanamwacha aketi, mchafu. Anaitwa "roho mchafu."

115 Mnakumbuka, Yesu aliwaambia, siku moja, wakati waliposema, "Mtu huyu anafanya hivi kwa Beelizebuli," Yeye alisema, "Mkisema hivyo dhidi Yangu, mtasamehewa. Lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja, kufanya jambo lile lile, na, neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe." Mnaona? Haya basi. Yesu akiwa na miguu michafu. Ungeweza kuwazia hilo? Ungeweza kuwazia, watu waliodai kumpenda Mungu, nao walikuwa wamechanganyikiwa sana katika kanuni zao za imani, na madhehebu yao na itikadi?

116 Yesu alisema, "Mapokeo yenu, mlilitangua Neno la Mungu." Huyo hapo, hapo, nalo Neno lilikuwa likitenda kazi, kwa kuwa lilikuwa limefanyika mwili, nalo lilikuwa likithibitisha kabisa kwamba Yeye alikuwa ni Kristo. Nao watu, pamoja na mapokeo yao, wasingeliacha litende kazi juu ya watu wengine. Hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya, akijaribu kulionyesha waziwazi. Basi, mnaona, hawakuamini Yeye alikuwa ni nabii.

117 Na, hata hivyo, Biblia ilisema angekuwa ni nabii. Biblia, Musa alisema, "Bwana Mungu wako atawaondokeshea nabii," Kumbukumbu la Torati 18:15. Nayo Biblia ilibashiri kile Yeye angefanya hasa. Naye huyu hapa anakuja, akikifanya miongoni mwa watu hao.

118 Na leo hii tunamwacha akiwa na jina chafu kama alilokuwa nalo wakati huo; tunawaacha waseme mambo dhidi Yake. "Nazo siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho," wakati Biblia ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nasi tungali tunaona aibu kusimama na kusema kitu kulihusu. Tunauonea aibu ushuhuda wetu ambao tu—tunadai kuamini. Badala ya kumwosha, kujaribu kumwosha kwa machozi ya furaha, kwamba Yeye yupo hapa, tunamwacha tu aketi, mchafu. "Sitahusika nalo. Sishirikiani na kitu kama Hicho, sitakigusa kwa mkono wangu." Mnaona?

119 Haya basi. Ni kundi lile lile la Mafarisayo, chini tu ya jina lingine. Tunamwacha tena aketi namna hiyo, kwa sababu ile ile, hatuamini kwamba Yeye ni nabii. Tunalionea aibu. Kwa nini? Sababu ile ile. Hatuliamini. Watu hawaliamini. La, bwana.

120 Yeye anaweza akaja, afanye lolote atakalo; wameshika njia zao, wala hakuna haja ya kujaribu kujipumbaza nao. Nanyi mwajua, Biblia ilisema wangekuwa hivyo. Kweli kabisa. Biblia ilisema wangekuwa hivyo, "Vuguvugu, mfano wa utauwa, bali hawana nguvu zake." Mnaona? Hiyo ni kweli.

121 Tunajiunga na kundi hili la kielimu, lililopigwa msasa linalosimama pale, na tukiwa na ujamii wetu mkubwa na nyakati, na makanisa yetu mazuri, na mapambo mazuri. Ndipo Yesu Kristo anaweza kuingia, nanyi mnamwacha akae mchafu. Neno linaweza kudhihirishwa miongoni mwetu, nasi tungali tunatembea huku na huku, tunawaacha watu waongee juu Yake. Loo, jamani!

122 Lakini, mwajua, kuiharakisha hadithi yetu, hebu tubadilishe onyesho usiku wa leo. Hebu tuelekeze kamera zetu upande mwingine, huko chini kabisa kichochoroni, maskini kichochoro kichafu, huko juu kabisa juu ya chumba kidogo cha kale kilichofungwa kwa ufito. Mlango unafunguliwa, na mwanamke anatoka nje. Vema, hakupendwa sana miongoni mwa watu. Alikuwa ni mwenye dhambi, naye alijipatia riziki kwa njia mbaya. Kwa hiyo anatoka nje polepole, anashuka kwenye maskini vipandio vyenye sauti ya mkwaruzo. Anaingia

kichochoroni. Kisha anashuka chini, kupitia kwenye mapipa ya takataka, ndipo anaingia mtaani.

123 Mbona, hakuna mtu huko nje, kwa hiyo anaanza kushangaa ni . . . "Loo, nakumbuka. Farisayo huko juu, Mchungaji Farisayo, anafanya dhifa kubwa. Kila mtu yuko kule. Biashara itakuwa mbaya leo." Kwa hiyo, anazurura mtaani. Ndipo anapoanza kutembea, na kusema, "Vema, itanibidi kungojea mpaka hiyo itakapokwisha." Naye alipata riziki yake kwa njia mbaya. Kwa hiyo, alikuwa anatembea mtaani.

124 Basi baada ya kitambo, maskini tumbo lake lenye njaa likanusia hiyo nyama choma ya kondoo. Akawaza, "Jamani, harufu nzuri hiyo! Kamwe sijapata kula kitu kama hicho, maishani mwangu." Labda alikuwa amefukuzwa, akaenda mtaani, wakati, na wazazi fulani.

125 Unajua, mara nyingi tunawazia juu ya utovu wa nidhamu wa vijana. Nafikiri mwingi sana ni uhalifu wa wazazi. Watoto hao wangalifunzwa kuomba na kumtumikia Mungu; badala ya mama huko nje mahali fulani kwenye karamu ya anasa, na karamu zake za kidini; naye baba yuko huko kwenye uwanja wa gofu mahali fulani; naye dada yuko huko nje na mtoto, huko nje mtaani, wakizurura. Labda mambo yangalikuwa tofauti kama wangalikuwa na madhabahu ya mtindo wa kale ya maombi, Biblia badala ya jozi ya karata. Na kuitupilia televisheni hiyo nje ya mlango, zamani sana, basi huenda ingalileta tofauti kubwa. Ninyi nyote, ilikuwa ni vibaya kwenda kuona sinema. Ibilisi akaiweka moja kwa moja juu yetu. Akaileta moja kwa moja nyumbani mwao. Mnaona? Mnaona?

126 Alikuwa na njaa. Akainusa hiyo. Akasema, "Jamani! Inanukia vizuri. Sijui kweli kipande cha nyama choma ya kondoo kingekuwa na ladha gani katika kinywa cha mwanadamu? Si—sijui jinsi kingekuwa. Ninaamini nitasogea tu kule."

127 Sasa, asingeweza kusogea karibu sana nao, maana alikuwa ni mwanamke mchafu. Walikuwa wanaojihesabia haki, mnaona. Wote walikuwa ni wa kanisa. Kwa hiyo, wasingeweza kukaribia walipokuwa. Alihesabiwa kuwa mwenye dhambi.

128 Kwa hiyo, wakati akisogea karibu, na kuweza kuangalia huku na huku, akawaona wote wamesimama pale, huku wanameza mate, wakati wakitweta, mwajua, na kumwangalia huyu kondoo dume, ama mwana-kondoo, mle ndani akichomwa. Na chakula chote kizuri kikipakiwa mle. Ni wakati mzuri jinsi gani!

129 Basi akaanza kuangalia kwenye umati jinsi hiyo, ndipo macho yake yakamwangukia. "Ni nani Yule? Ana miguu michafu. Sijui Yule ni nani . . . Yuko wapi mtu angaliweza kuniambia? Aisee, hivi wewe . . ." Anageuka upesi sana, hataki kujihusisha naye. Yeye ni mwenye dhambi. Kwa hiyo,

akamwuliza mtu mwingine, hatimaye, labda maskini mama aliyekuwa akiamini na kungalia vile vile. Kasema, "Bi mkubwa, ungeninii . . . Samahani. Lakini ungeninii . . . Ni nani yule anayeketi pale? Alininii namna gani . . . mtu yule."

130 "Vema," wakasema, "unajua Yule ni nani? Je! uliwasikia wakinena juu ya yule Yesu wa Nazareti, anayedhaniwa kwamba ni nabii?"

"Loo, naam. En-he. Huyo Ndiye?"

"Huyo Ndiye."

131 "Vema, Yeye hajaoshwa. Nilisikia ya kwamba kila mtu anapaswa kuoshwa kabla hawajaingia kule, na kupakwa mafuta. Hebu mwangalie. Vema, si sawa."

132 Alikuwa na fursa imejitokeza. Akakumbuka hadithi ambayo mtu fulani alimwambia. Mwanamke mwingine mwenye shughuli kama yake, wakati mmoja, huko Sa—Samaria, mji wa Sikari, aliyekuwa amesamehewa kila dhambi. Naye akatambua ya kwamba huenda hiyo ikawa ni nafasi yake. Kwa hiyo atamfikiaje sasa? Aliona kwamba alikuwa ni mhitaji, naye alitaka kumtumikia, wala asingeweza kumfikia. Hivyo ni kama ilivyo. Kwa hiyo akawaza, "Nifanyeje? Hajapakwa mafuta. Miguu Yake ni michafu. Hakuna anayemjali. Loo, laiti ningaliweza kuingia mle ndani!" Huyo ni moyo wa toba kwelikweli. "Laiti ningaliweza kumfikia!" Sasa, yeye anawazia, kufikia . . .

133 Moyo wake unashika kitu fulani. "Unajua ninaloamini nitafanya? Ninajua."

134 Huyo anashuka kwenda barabarani, upesi tu awezavyo, kupitia kichochoroni, anapanda vipandio hivi vya kale vyenye mkwaruzo, na kufungua mlango. Anaingia mle na kuchukua ki—kifuniko cha stokingi, mwajua, na kukitoa, anahesabu ana pesa ngapi. Akasema, "Mimi, je! hizo zatosha kununua mafuta ya kupaka? Hebu tuone kama imetosha. Kuna vipande ishirini vya Dinari ya Kirumi. Labda hizo zimetosha. Lakini, hebu kidogo, siwezi kufanya hivyo. Yeye ni nabii, Naye atajua ambapo nilizipata hizo pesa. Atajua jinsi nilivyozipata. Kamwe siwezi kufanya hivyo." Kwa hiyo, labda alizirudisha, tena.

135 Basi alipozirudisha, kuna kitu fulani kilichoendelea kuuzungumzia moyo wake. "Lakini hivi ungemwacha aketi pale mchafu, namna hiyo? Ungemwacha Mtu pekee ambaye anaweza kuziondoa dhambi zako, aketi mchafu, wakati ambapo unaweza kumhudumia?"

Kwa hiyo anajiambia, "Ajue asijue, ninaenda."

136 Basi akashuka kwenda barabarani na kuingia dukani ambamo mna maskini jamaa mwenye pua iliyopinda ameketi pale. "Na, vema, wataka nini hapa?"

137 Akasema, “Ninataka marimari yenye marhamu mazuri kuliko yote uliyo nayo. Sio ya bei ya chini zaidi, nataka iliyo bora kuliko yote.” Alikuwa na sababu maalum.

138 Na hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Inatupasa kumpa chetu kilicho bora kuliko vyote, kila kitu tulicho sisi, maisha yetu ya ujana, sio kungojea mpaka tutakapokuwa wazee na tunakufa. Tumpe Yeye, kilicho bora kuliko vyote tulivyo navyo.

139 Na hapo akapata yaliyo bora kuliko yote. Akaenda hapo, kasema, “Hebu tuone ni pesa ngapi hizo. Unazo hizo fedha, kwanza.” Yeye alimjua, pia. Kwa hiyo akasema . . . Naam, alikuwa na fedha. “Hivi, unayapeleka wapi haya?”

“Nimeyanunua kwa haja maalum.”

140 Kwa hiyo, anapanda kwenda. Sasa, hana mwaliko. Lakini ataingiaje? Lakini, kwa namna fulani, kama ukitaka kumhudumia Yesu, atakufanyia njia ya kuingilia. Kwa njia moja au nyingine, akaingia.

141 Basi huyo hapo Yesu, ameketi pale, bado. Basi ilitokea aliwazia wakati alipoingia mle, moyo wake ukidunda upesi sana, “Loo, jamani! Vipi kama ikitokea kuwa hataniruhusu?” Kuna mambo mengi sana ya kuwazia. “Vipi kama angekuja huku na kusema, ‘Aisee, ewe mwanamke mchafu, unafanya nini hapa Mbele Zangu? Hivi hujui kwamba Mimi ni Mwana wa Mungu? Haikupasi kuwa hapa Mbele Zangu’?” Moyo wake ulikuwa karibu kuzimia. Naye akawazia, “Nifanye nini? Lakini sina budi kwenda Kwake. Siwezi kupitisha wakati huu. Hii huenda ikawa ndiyo nafasi ya mwisho nitakayokuwa nayo.” Na huenda ikawa yako, pia. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

142 Akaangalia chini, ndipo moyo wake ukaanza kuvimba. A—alijua alikuwa Mbele Zake. Kuna jambo linalotukia unapofika Uweponi Mwake. Akaona machozi yakianza kutiririka mashavuni mwake. Naye alikuwa amesimama pale, anatetemeka, akiwa na chupa hii mkononi mwake. Ndi—ndipo akaanguka miguuni Pake. Naye akawaza, “Siwezi kuangalia juu. Mimi nina hatia sana na ni mchafu, siwezi kuangalia juu.” Kwa hiyo akaanza kulia. Yakaanza kutiririka miguuni Mwake. Naye akaanza kuiosha, namna *hiyo*, kwa mikono yake; kuipangusa, akijaribu kuyapangusa machozi miguuni Mwake, na kuiosha miguu Yake kwa machozi yake. Na baada ya kitambo kidogo . . .

143 Hakuwa na taulo ya ku—kuipangusa miguu Yake. Kwa hiyo, nywele zake zilikuwa zikining’inia chini, naye akaanza kuipangusa miguu Yake kwa nywele zilizokuwa kichwani mwake.

144 Hivi dada zetu wasingekuwa na wakati mgumu sana kufanya hivyo? Ingewabidi kusimama kwa kichwa chao kufanya hivyo. Mnaona? Hakika. A-ha. Dada zetu, leo hii. Sijui kama, ninyi, sijui kama wanawake wanatambua ya kwamba Mungu

hutimiza ahadi Zake zote. Sijui kama mnatambua ya kwamba haiwezekani kabisa kwenu kuingia, namna hiyo. Yeye hutimiza ahadi Zake zote. Je! mnatambua mnalofanya wakati mkifanya hivyo? Mnaukataa wema. Biblia ilisema, ya kwamba, "Kama mwanamke akikata nywele zake, lilikuwa si jambo la kawaida kwake hata kuomba. Naye anamkosea heshima mumewe, kwa kufanya hivyo."

145 Basi kumbukeni, mwanamke ndiye aliyevunja amri moja ya Mungu, ndiye aliyesababisha haya yote kutokea. Mnadhani mtu akivunja moja, ataingia tena? Wazieni hilo. Labda, wakati mwingine, wahudumu hawana ujasiri wa kutosha kuwaambia. Huu ndio wakati mmoja mtakaolisikia. Ni Kweli.

146 Mtu fulani alisema, "Mbona usiachane na hao wanawake?" Mtu mashuhuri aliniambia hilo, sio muda mrefu uliopita. Kasema, "Vema, wanaamini kwamba wewe ni nabii. Wafundishe jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu, na kuyapata mambo haya makubwa mno, na jinsi ya—ya kuwa manabii," na kadhalika. Nikasema . . . "Ati kuwafundisha mambo makuu zaidi."

147 Nikasema, "Nawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatasoma ABC zao?" Inaonyesha. Ya nje huonyesha yaliyo ndani. Bali mnaendelea, mnalifanya, kwa vyovyote vile. Ni kwa nini? Hamna habari.

148 Huyo hapo. Kwa nywele zake, akaanza kuipangusa miguu Yake kwa hizo, na kuikausha miguu Yake. Alikuwa anaogopa kabisa. Ndipo baada ya kitambo kidogo, akaitwaa chupa hii ya manukato, akaivunja, naye akajaribu kuipiga na kuivunja. Na kuimimina miguuni Mwake. Naye alikuwa akilia. Na kila alipolia, angeinama na kuibusu miguu Yake. Akapatwa na mpagao.

149 Unapofika Uweponi Mwake, inakufanya kupagawa. Nilipagawa. Mtu yeyote anayeenda Uweponi Mwake, anayemwamini na ana imani Naye, itakufanya upagawe. Kwenye siku ya Pentekoste, wakati alipokuja katika umbo la Roho Mtakatifu, walipagawa. Wakati unapoamini kweli, nawe unajua na unatambua ni nafasi yako, nawe uko Mbele Zake, una hakika nalo.

150 Akafanya [Ndugu Branham anatoa sauti ya kubusu—Mh.], akaibusu miguu Yake, na kulia, na kuiosha, na kuipangusa, na [Ndugu Branham anatoa sauti za kubusu.] na kuibusu miguu Yake tena. Mwajua, Yesu, kama angaliusogesha mguu mmoja, huyu angalitimua mbio na kuondoka pale. Lakini, wajua, Yeye aliketi tu na kumwacha afanye hivyo.

151 Mwajua, kama unataka kufanya jambo fulani, kwa kuwa anakuacha ulifanye. Huenda ikakiuka utaratibu kabisa, bali atakuacha ulifanye, kwa vyovyote vile. Mnaona? Naye . . .

152 Ilikuwa ni kumtumikia, naye alikuwa akiitawadha miguu Yake. Naye akaketi tu pale na kumwangalia. Aliogopa kuangalia

juu, maana aliogopa atamfanya aambae. Na, mnaona, alikuwa akiitawadha miguu Yake. Ni nafasi ya kumfanyia jambo fulani. Naye alikuwa . . . Sasa, mnaona, basi wakati Yeye . . .

153 Wakati Yesu alipomjibu yule Farisayo, Yeye alimhesabia haki kwa kazi yake. Bali alipomhesabia haki yeye binafsi, alimhesabia haki kwa imani yake, "Imani yako imekuokoa." Alimwonyesha Farisayo huyo kuwa matendo yake yalikuwa ni kitu gani.

154 Kwa sababu, matendo yako huonyesha imani yako. Sasa acheni nywele zenu zikue. A-ha! Mnaona? Vema. Sasa, mnaona, inaonyesha kile unachoamini, ama huamini. Hilo ni Neno la Mungu. Hakuna Maandiko katika Biblia ila lililo Kweli. Kwa nini mnafanya hilo? Sasa angalieni, Hollywood chungu nzima katika Pentekoste, hiyo ndiyo shida. Sasa tunaona. Hiyo ni Kweli. Ni Hollywood chungu nzima. Mnayaangalia mambo haya na kuyaiga.

155 Mama mmoja aliniambia, sio muda mrefu uliopita, kasema . . . amevaa maskini nguo ndogo, iliyombana sana. Nikasema, "Mbona usiitoe hiyo, kwa kuwa wewe ni dada?"

156 Naye akasema, "Mbona, Ndugu Branham, hawatengenezi nguzo zingine zozote."

157 Nikasema, "Wanatengeneza cherahani, na wana vitambaa. Unaona? Unataka tu kuivaa."

158 Nitawaambia ni kwa nini. Hebu niwaambie, enyi dada. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] En-he. Asanteni. Moja ya siku hizi itawabidi kuwajibika kwa kufanya uzinzi.

159 Unasema, "Vema, Ndugu Branham, mimi ni safi tu kwa mume wangu niwezavyo kuwa." "Mimi ni safi kwa mpenzi wangu mwanamume." Hilo laweza likawa ni kweli, pia.

160 Lakini Yesu alisema, "Kila amwangaliaye mwanamke, kwa kumtamani, tayari amefanya uzinzi pamoja naye moyoni mwake." Na endapo ulijianika huko nje, naye huyo mwenye dhambi anawazia hilo juu yako, kwa kuwa ulijianika; kwenye Siku ya Hukumu, wakati yeye atakapowajibika kwa kufanya uzinzi, mwenye hatia ni nani? Wazia hilo. A-ha. Ni kweli kabisa. Loo, enyi wanawake, rudini, akina dada, rudini kwa Kristo; ndugu, fanyeni vivyo hivyo. Nanyi wanaume mtakaowaacha wake zenu kufanya hivyo, na ati unajiita mwanamume, kichwa cha nyumba? En-he. Angalia. Tuko kwenye wakati mbaya sana, rafiki, nasi tunaona.

161 Na hapa alikuwapo maskini mwanamke huyu akiibusu miguu Yake, na kuiosha miguu Yake, na kuipangusa kwa nywele zake za kichwa chake. Na mara, maskini Farisayo, huko pembeni, alitokea kwamba aliona hilo. Loo, jamani! Hasira yake ya mwenye haki ikapanda, na—na kidevu chake kikubwa kikavimba, nao uso wake ulionekana kana kwamba

utapasuka. "Loo, jamani!" Akasema, "Njoni hapa. Angalieni hapa. Angalieni pale."

162 Ndipo akasema moyoni mwake mwenyewe sasa, ni—niani mwake, akasema, "Kama mtu yule angekuwa ni nabii, angejua ni mwanamke wa aina gani huyo aliyemgusa."

163 Tuone kama Yeye ni nabii, au la. Mnaona, Yeye alijua mawazo yaliyokuwa moyoni mwake. Ndipo mara, akasogea. Ndipo maskini mwanamke yule akasimama, kuangalia juu, macho yake yanatokwa machozi. Akaangalia huko, na Yeye akasema, "Simoni," akasema, "Ni—ni—nina neno la kukwambia." Loo, jamani! "Haya basi, Simoni. Nina jambo la kukwambia. Ulinialika hapa. Nilikuja kwa mwaliko wako. Wewe ulinialika. Na wakati nilipofika mlangoni, hukuiosha miguu Yangu. Kisha nilipoingia, hukunipaka kichwa changu mafuta. Uliniacha niingie, mchafu. Wala hukunikaribisha kwa busu, ingawa ulinialika. Lakini mwanamke huyu hapa, acha awe chochote awezacho kuwa, ameiosha miguu yangu kwa machozi yake. Ameipangusa kwa nywele za kichwa chake. Pia ameipaka miguu yangu mafuta, na hakuacha kuibusu miguu Yangu tangu amekaa pale." Alijua kama alikuwa ni nabii, au la.

164 Ndipo akasema, "Simoni, ninataka uangalie jambo fulani." Akasema, "Ni kitu gani . . . Nataka kukupa fumbo." Kasema, "Mengi yakisamehewa, upendo ni mwingi." Ndipo akampa msemo huo. Naye Simoni akamjibu.

165 Angalieni. Simoni hakumpa chochote cha kuoshea miguu Yake, lakini alikuwa na maji mazuri sana yangaliweza kuwako. Wazieni tu, machozi ya mwenye dhambi aliyetubu yakiosha uchafu kutoka kwenye miguu ya Yesu; machozi ya macho ya mwenye dhambi yakiosha uchafu kutoka miguuni Mwake.

166 Loo, enyi wanaume na wanawake, usiku wa leo, mnapoiona shutuma ya Injili! Nasi ni baridi sana, ingeondoa vipodozi vyote usoni mwetu kama tungalilia machozi; nasi tungeonekana wenye sura mbaya sana, kwenda barabarani. Utakuwa nini utakapokabiliana na malango ya Mbinguni huko ng'ambo?

167 Naye huyo hapo. Alikuwa ameitawadha miguu Yake, akaibusu miguu Yake, kisha akampaka mafuta, na kufanya yote aliyoweza, kwa maana alitaka msamaha. Mara, a—akashangaa Yeye atafanya nini sasa.

168 Alikuwa amemwonyesha Simoni, nalo likamwendea upogo. Jambo alilosema, "Yeye hakuwa nabii," ilithibitika kwamba alikuwa nabii, kwamba alikuwa ni Neno la Mungu. Sasa, amesimama pale huku uso wake umevimba. Angalimshika kwa nguvu maskini mwanamke huyo, akamtupe nje ya kanisa.

169 Lakini alikuwa amepata alichoomba. Amina. Haileti tofauti yoyote yale hao wengine waliyosema. Alipata alichoomba.

170 Sasa anamgeukia. Maskini moyo wake mdogo ukaanza kudunda upesi sana. Sasa Yeye atasema nini? Huyo hapo. Vipilipili vyake vyote vya kupendeza vilikuwa vimening'inia chini hata kiunoni mwake hapa. Nayo macho ya—yake yalikuwa yakidondosha machozi. Nao uso wake na midomo yake imejaa mafuta, ambapo alikuwa akiibusu miguu Yake, baada ya kumpaka hayo mafuta. Hakika alionekana amechafuka. Lakini hayo macho makubwa sana, yakiangalia yaone atakachosema.

171 Akasema, "Nami namwambia: dhambi zake zote, ambazo ni nyingi, zimesamehewa." Jambo ndilo hilo. "Dhambi zake zote zimesamehewa."

172 Hilo ndilo ninalotaka kusikia. Loo, hayo ndiyo maneno ninayotaka. Sijali kile hao wengine wanasema. Niko tayari kusimama katika dhehebu lake, nitangaze ya kwamba Yeye ni Neno la Mungu. Sijali wanachosema. Acha walitie uchafu wowote watakao, wakisema, "Msomaji wa mawazo, mpiga ramli," chochote watakacho. Niko tayari kuibusu shutuma hiyo kutoka Kwake. Ni Neno Lake. Hakika. Aliliahidi. Yeye ni Neno leo kadiri alivyokuwa wakati huo. Alisema hivyo.

173 Sasa, ewe rafiki, huenda ikawa wapo watu wanaoketi hapa ambao hawawezi kukubali kwamba Yeye ni Nabii. Huenda usikubali kwamba Yeye ni mponyaji. Bali kuna jambo moja ambalo kila mfuasi wa kanisa anapaswa kukubali, Yeye ni Mwokozi.

174 Nami nataka kusema jambo hili kabla ya kufunga. Sio muda mrefu uliopita, wakili rafiki yangu alikuwa akifanya kesi ya mwanamume na mwanamke ambao walitaka kutengana. Wakili huyo alikuwa ni Mkristo muungwana. Akasema, "Msi—msitengane." Alijaribu alivyoweza wasitengane. Lakini, la, walikusudia kutengana. Kitu fulani kilizuka kati yao. Basi baada ya kitambo kidogo, akasema, "Vema, endapo mna nyumba huko chini, afadhali mwende kule, mkagawanye mali. Maana, kama itawabidi kwenda kule, hao wanasheria na kadhalika wakiingilia, mnajua litakalotukia. Watachukua kila moja ya hiyo."

175 Kwa hiyo wakaingia vyumbani, wakagawane kile walichokuwa nacho. Wakaingia ukumbini. Wakagombana na kuzozana. "Nilinunua *hiki*," na "Nilikuwa na *hiki*." Nao wakaendelea, katika chumba kingine, nao wakagawana mle ndani. Basi hatimaye wakapanda darini. Walikuwa na... Wakakumbuka walikuwa na kasha la kale kule juu. Wakaingia mle na kuanza kusema, "Vema, *hii* ilikuwa ni ya mamangu." "*Hii* ilikuwa ya mamangu," namna hiyo. Wakafikia kwenye hilo kasha, kila mmoja, wote wawili wamepiga magoti sakafuni, huku mlango wa hilo kasha ukiwa wazi, wakigawana kipi ni cha nani. Wasingekubaliana. "*Hicho* ni changu." "Nililipia *hicho*."

"Mimi nilifanya kazi." "Nilikaa nyumbani wakati ukiifanya," wakigombana.

176 Hatimaye wakainua kitu kingine, na wote wakakishika ghafla, wakati ule ule. Kilikuwa ni kitu gani? Jozi ndogo ya viatu kutoka kwa mtoto mchanga aliyezaliwa kwenye ndoa hiyo, ambaye Mungu alimtwaa. Wasingeweza kubishana. Walikuwa na kitu kimoja shirika. Wakati wakishikana mikono, yeye alikumbuka kwamba huyu alikuwa ndiye mama wa mtoto huyo. Mume akakumbuka kwamba huyu alikuwa ndiye mama. Naye mke akakumbuka huyu alikuwa ndiye baba. Na huku wameshika maskini vijiatu hivyo mikononi mwao, walivutana, wakakumbatiana. Hiyo kesi ya talaka ikabatilishwa. Kwa nini? Walipata kitu walichokuwa nacho shirika.

177 Huenda hukukubaliana nami juma hili, kumwona Roho Mtakatifu akiingia, kuthibitisha Maneno haya na kadhalika. Fanya ninii . . . Huenda usikubaliane na hilo. Huenda usikubaliane na wagonjwa kuponywa. Bali tuna kitu kimoja shirika: hicho ni Damu ya Yesu Kristo inayotuokoa na dhambi. Je! utaosha uchafu kutoka miguuni Mwake usiku wa leo?

178 Na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Kumbukeni, Yeye hutimiza kila ahadi. Yeye hutimiza kila ahadi. Aliahidi, "Ingawa dhambi zako ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji. Dhambi zako zote umesamehewa, kama utaamini tu."

179 Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Sijui ni wangapi hapa watainua mkono wenu na kusema, "Ndugu Branham, ninataka, maishani mwangu mwote, ninataka kutomfanya aketi na kuaibishwa. Nami ni—nina nafasi kama maskini mwanamke yule aliyokuwa nayo. Ninataka, kwa ushuhuda wangu, kuosha uchafu kutoka Kwake, ninii . . . Jina Lake la thamani"? Waweza kuinua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham. Na—na . . . "? Mungu awabariki. Mungu awabariki. Hilo ni sawa.

180 Sasa, Baba wa Mbinguni, kulikuwa na mikono mingi, mingi iliyoinuliwa hapa sasa hivi. Nasi tunaona ya kwamba Jina la Yesu Kristo limekanyagiwa mavumbini. Na kila kitu Mbinguni kimeitwa Hilo. Kila kitu duniani kimeitwa Hilo. Kila—kila mfuasi wa kanisa, kila mshirika wa Mwili wa Kristo, ni Bibi Yesu. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba tutaona na kufahamu hilo, usiku wa leo. Na jalia neema Yako ije juu ya watu hawa sasa na kuwasamehe kila dhambi, wapate kujua ya kwamba, katika Uwepo Wako sasa, na kujua kwamba Wewe upo hapa. Jalia Roho Wako Mtakatifu atufundishe sisi sote sasa, na jalia tusamehewe dhambi zetu zote na makosa yetu. Na tangu usiku huu na kuendelea, jalia tuwe viumbe vipya, waliojazwa na Roho Wako. Tujalie. Na tuuhisi Uwepo Wako. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake.

181 Na wakati tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu. Sijui, usiku wa leo. . .Sasa, ninazungumza na wenye dhambi, pamoja na wafuasi wa kanisa, na waliorudi nyuma, na hao wasio na Roho Mtakatifu. Ninazungumza nanyi. Kwa nini Farisayo hakumkubali?

182 Tutaendelea kumwita. "Ee Bwana, utakuja?" Wakati mtoto wako mchanga alipokuwa mgonjwa, ulimwita. Yeye alikuwa na rehema, hapana shaka. Ulipokuwa karibu kupata ile ajali pale, ulimwita. A—akakujalia utoke humo. Lakini sijui, sijui tu, pamoja na mambo haya yote tumwombayo, na kumwalika, halafu ajapo kutuzuru namna hii, sijui kama tunaona tu aibu.

183 Kusema, "Vema, nimekuwa mfuasi wa kanisa, bali ninataka kumpata katika ubatizo wa Roho Mtakatifu usiku wa leo. Ninamtaka. Ninamhitaji. Sijali yale walimwengu wengine wanasema kulihusu. Ninamtaka." Ungetaka kuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu? Kama ungetaka, nitakuomba ufanye jambo fulani. Ninakutaka uje hapa, papa hapa nilipo sasa. Shuka huku chini na kusimama kwenye shimo hili papa hapa karibu nami. Kila mtu humu ndani, kila mtu asiyeokoka, kwanza, waweza kuja hapa na kusimama hapa kwa dakika moja tu?

184 Kama unaamini kwamba Yeye huyasikia maombi, waweza kuja hapa na kusimama hapa kwa dakika moja sasa, wakati tukiimba kifungu kimoja cha wimbo? Ni kitu gani hicho? *Kwa Upole na Upendo Yesu Anaita*. Vema, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kila mtu akiomba, njoni moja kwa moja huku na msimame hapa, moja kwa moja hapa chini kwenye shimo hili hapa.

Kwa upole na upendo, Yesu. . .

Njoo, sivyo, ewe rafiki, popote ulipo?

Anakuita wewe na. . .

185 Yesu katika siku hizi za mwisho, kabla tu ya kuonekana Kwake katika umbo la mwili sasa, ameketi na miguu michafu. Je! uko tayari kuja kuchukua msimamo wako, kuondoa shutuma kutoka kwenye Jina Lake?

Anakuita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani.

Njoo nyumbani.

186 Hivi. . .Amka upesi sasa. Kata kauli. Njoo moja kwa moja sasa. Tuna wakati mwingi sana. Kesho ni Jumapili. Shule ya Jumapili haianzi hadi saa tatu na nusu. Njoo sasa.

. . .mliochoka, njoni nyumbani;

Kwa upole, upendo. . .

Je! mnatambua Yesu yupo hapa?

Anakuita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani.

Njoo nyumbani.

187 Hiyo ni kweli. Njoni kutoka kwenye roshani. Tutawangojea. Njoni moja kwa moja huku, kila mmoja sasa, na kuchukua mahali penu papa hapa chini. Sasa ninii tu . . . Hii inamaanisha maisha yako.

188 Ni kitu gani kinachotukia? Angalieni matetemeko ya nchi kote duniani, yakiitikisa dunia tena. Angalieni kinachotukia kila mahali. Wakati umekaribia. Na angalieni, mlango utafungwa, baada ya kitambo kidogo, nanyi mtalia mpate kuingia, wala hamwezi.

189 Nilizungumza na msichana mmoja, wakati fulani uliopita. Nilikuwa nikifanya mkutano katika kanisa la Kibaptisti, nami nikamwomba usiku huo amjie Kristo. Naye asingemjia. Halafu baadaye, alikutana nami hapo nje na kusema, "Kamwe usiniaibishe namna hiyo tena." Mwaka mmoja baadaye, nilipitia mtaani. Alikuwa ni msichana wa heshima. Nikapitia mtaani. Sketi yake ya ndani ikining'inia chini, akivuta sigara, akishuka kwenda mtaani. Alikuwa binti wa shemasi. Nami nikasema, "Aloo, hapo. Hivi . . . "

Akasema, "Aloo 'hubiri!" Lugha ya mtaani namna hiyo, "Aloo, 'hubiri!"

Nikasema, "Hivi huoni haya, sigara hiyo?"

190 Akasema, "Hei, ungetaka kinywaji kidogo kutoka chupani mwangu?" Alikuwa nusu mlevi.

Nami nikasema, "Hivi hujionei aibu?"

Akasema, "Njoo hapa. Ninataka kukupeleka mahali ninapoishi."

Nikasema, "Kwani huko nyumbani?"

"La."

Nikasema, "Kwani kuna nini?"

Akasema, "Kunywa kidogo kutoka kwenye chupa yangu. Nitakwambia."

191 Nikasema, "Hivi hujionei aibu, kunipa kinywaji kutoka kwenye chupa, ama sigara?"

192 Akasema, "Nataka kukwambia jambo fulani, mhubiri. Unajua usiku ule uliponiambia hiyo ilikuwa ndiyo 'nafasi yangu ya mwisho'?"

Nikasema, "Naam, nakumbuka."

193 Akasema, "Ulisema kweli." Akasema, "Tangu wakati huo, nafsi yangu imekuwa ngumu sana!" Akasema . . . Sasa hili hapa tamshi lake. Linatisha tu kabisa. Alisema, "Ningeweza kuiona nafsi ya mama yangu ikikaangiwa kuzimu kama chapati maji, na kuicheka."

194 Ungetaka kufikia kiwango hicho? Kamwe usimkatae. Kwa hiyo sasa hivi, mbona usije, usimame hapa pamoja na hawa wengine?

Njoo nyumbani, njoo nyumbani.

195 Kumkataa, hilo ndilo lililotukia. Kumbuka, utamkataa, mara ya mwisho.

Njoo nyumbani. Kwa upo-. . .

196 Yeye hutimiza miadi Yake yote. Nawe una moja Naye. Utakutana Naye kwenye ile Hukumu ama ukutane Naye hapa.

Anakuita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani.

197 Mwajua, nimeshangaa sana. Moyo wangu unajisikia kiajabu. Niliwaza, leo, nilipokuwa nikiomba. . . Nilikuwa na ujumbe mwingine ambao nilikuwa niuzungumzie. Yeye aliniambia nifanye hivyo. Aliniambia niseme hivyo. Nilifikiri kila mwanamke aliyekata nywele zake angekuwa amesimama hapa kwenye wito wa madhabahuni. Mnaona, unakuwa tu mgumu na mbali sana. Mnaona? Unapita mstari huo katikati ya wimbi hilo, unaona, pasipo kulisikia Neno la Mungu. Nilifikiri hakika lingetendeka. Lakini nadhani wakati umeenda kuliko ninavyodhania hasa. Kumbukeni, hiyo damu haiko mikononi mwangu. Sijajiepusha na kuwatangazia habari za Kusudi lote la Mungu, jinsi lilivyo.

198 Kumbukeni, kuna kitu fulani ndani, kinachotambulisha upande wa nje. Kiondokee, ewe dada, mpendwa. Ndugu, mshike mkono na mje huku juu. Mbona usije? Hivi hutakuwa, hivi hutaki kuwa Mkristo halisi? Kuna haja gani ya kuishi maisha nusu-nusu, na kuishi chini ya hukumu? Usifanye hivyo. Unaona? Unasema, "Vema, ni—ni-. . ." Sijali umefanya nini. Matunda yako ndiyo yanayokutambulisha.

199 Ninasafiri kote Marekani, mara kwa mara. Na kila mwaka ninapovuka, inazidi kuwa mbaya zaidi na zaidi, kwa hiyo ninajua kuna kasoro. Siku ya neema inapita. Msiache hilo liwapate hapa Tampa. Mko hapa kwenye jiji kubwa mno, ambamo kila kitu kimejaa madoido, kama vile tu Hollywood,

200 Ulimwengu mzima umechafuliwa. Yote yaliyo kwenye televisheni na kadhalika ni maskini upuuzi mchafu, wa kishenzi. Nanyi mnajaribu kuuiga namna hiyo. Hivi hutachukua mfano wa Yesu? Hivi huta—hutamruhusu? Hutalisikiliza Neno Lake? Hutafanya mambo haya yaliyo haki?

201 Ni wangapi humu ndani watakaosema kwa uaminifu kwamba unajua hujampokea Roho Mtakatifu? Jiangalie mwenyewe, kwenye kioo, na kujua hujampokea. Ujue, na uyaangalie tu maisha yako mwenyewe, na vile ufanyavyo.

202 Si kwa sababu wewe ni mfuasi wa kanisa, "Mimi ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpres-. . . Mimi. . ." Hiyo ni sawa. Sisemi kitu dhidi ya hilo. Lakini ninakuuliza, hivi unamjua

Kristo Yesu? Yeye anaishi ndani yako? Kama anaishi, Yeye atajitambulisha mle. Kama yuko mle, itambidi kujitambulisha. Huwezi kumficha, Yeye huonekana wazi.

203 Ukiwa huna Roho Mtakatifu, na unajua hunaye, inua mkono wako. Kuwa mwaminifu hivyo. Useme, "Sina Roho Mtakatifu. Ninajua sina." Mungu akubariki kwa uaminifu huo. Mungu atauheshimu uaminifu huo. Kama unamtaka Roho Mtakatifu, naomba uje usimame hapa pamoja na hawa sasa, hawa wenye dhambi waliotubu hapa. Hivi huwezi kuja wakati huu? Njoo huku na usimame, tunapouimba tena. Useme, "Ninamtaka, Ndugu Branham." Ninawaambia kwamba unahitaji Huyo. Itakulazimu kuwa Naye, kwa ajili ya Unyakuo. Hiyo ni kweli kabisa.

204 Sasa, kumbuka. Je! unaamini Mungu husema nawe? Unaamini huyo ni Yesu Kristo? Inua mkono wako. Kama unaamini, juma hili, umekuwa mikutanoni, unaamini ni Kristo. Vema, basi mahali pako ni madhabahuni.

205 Nanyi wanawake, aibu kwenu. Wanaume, aibu kwenu kwa kumwacha afanye hivyo. Ninyi wanaume huku, mnaofanya mambo hayo!

206 Na baadhi yenu ninyi wahudumu, hiyo dola yenye nguvu badala ya Neno la Mungu Mwenye Nguvu; mnaliachilia kusanyiko hilo liingie kwenye hali kama hiyo, kwa sababu tu ya dhehebu fulani.

207 Mnasoma Biblia ile ile ninayosoma. Hivi hamjionei aibu? Yesu na miguu michafu. Je! hamna ujasiri halisi wa Mkristo, kusimama na kulitetea Hilo? Inaonekana kana kwamba mngelitetea.

208 Mungu aturehemu. Ninaomba ya kwamba Mungu atamtuma Roho Mtakatifu kuwasadikisha sasa hivi, ambaye atalifanya kusanyiko hili litambue mahali lilipo.

209 Hivi unatambua ya kwamba hii ndiyo nafasi yako? Utafanya kama yule tarishi alivyofanya, kuiacha nafasi yako ya mwisho? Utafanya hivyo? Usifanye hivyo. Kukiwapo na shaka mahali popote, ama kitu kibaya, chukua mahali pako panapofaa papa hapa chini. Chukua mahali pako. Hapa ndipo mahali pako.

Unasema, "Vema, sitaki ninii . . . "

210 Wala, nao hawakutaka. Wangalienda kule na kumwona ameketi pale. Wangalikwenda na kujitambulisha wenyewe. Bali ilikuwa ni kinyume na kusanyiko lao. Vipi kuhusu . . .Haikuwa ni kinyume Chake. Maskini mwanamke huyo hakujali. Alijua alikuwa ni mwenye dhambi. Akapata msamaha.

211 Sijui kilichotukia. Wako wapi usiku wa leo? Yuko wapi mwanamke huyo, usiku wa leo, mnafikiri? Na Farisayo yuko wapi, usiku wa leo, ingawa ni wa kidini? Ungaliweza kuwasikia wote wawili, mahali walipo, hakika ungepachukua mahali pa

mwanamke huyo, wakati wowote. Kwa hiyo, hata uwe ni wa kidini jinsi gani! Kama unaninii . . . Yesu hutimiza kila miadi. Kila Amri, Yeye, inakubidi kuiwajibikia.

212 Kwa hiyo, afadhali uje sasa, kama huna Roho Mtakatifu. Alikuamuru uje. Yeye alisema, katika Kitabu cha Matendo, Petro alisema, alisema, "Tubuni kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Na mradi tu Yeye angali anaita, angali anamtoa Roho Mtakatifu.

213 Tunapoimba tena, mbona usije? Hiyo ndiyo mara yangu ya mwisho sasa. Kumbukeni, Kristo amekuwa hapa, nanyi nyote mkainua mikono yenu, mkatambua ya kwamba ilikuwa ni Yeye na Neno Lake.

Na chini, kwamba, Kristo, moyoni mwangu, amehuzunika.

214 Yesu aliketi juu ya Yerusalemu, wakati mmoja, kasema, "Yerusalemu, Yerusalemu, jinsi gani ningewafunika kama kuku awafunikavyo vifaranga wake, bali hamkutaka."

215 Mara nyingi, ninapokuja miongoni mwenu, kama nilivyowaambia asubuhi ya leo kwenye kiamshakinywa, ninyi Wapentekoste wazuri, na watu wa kila namna. Ninapokuja miongoni mwenu, Roho Mtakatifu aliye ndani yangu, akisema, "Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya. Jinsi kanisa lingekuwa limesimama siku hizi katika nguvu zake, bali hamkutaka." Mnaona? Hamkutaka. Mbona msifanye hivyo sasa? Huu ndio wakati. Wekeni kando kila mzigo unaoninii . . . ile dhambi iwazingayo kwa upesi. Na tupige mbio kwa subira katika mashindano yaliyowekwa mbele zetu.

216 Tunapoita mara nyingine moja, kila mtu aimbe pamoja nami sasa. Amka moja kwa moja uje huku. Kama huna ubatizo wa Roho, kama wewe ni mwenye dhambi, aliyerudi nyuma, chochote ulicho, njoo huku tukaombe pamoja. Hivi utakuja sasa? Huu ndio wito wetu wa mwisho.

Kwa upole na upendo Yesu anaita,
Anakuita wewe na mimi;
Angalia kwenye yale malango Yeye anaita na
  kungoja,
Akitungoja wewe na . . .

217 Vipi kama Farisayo angesikia wito huo wa madhababuni, usiku wa leo, akiketi huko nyuma, angefanya nini?

Njoo nyumbani, njoo nyumbani.

218 Yeye alitenda dhambi akamaliza safari yake, siku yake. Hivi utafanya vile vile? Vipi kama yule mvulana tarishi angeweza kusimama mbele Zake tena, jambo la kwanza lingekuwa ni nini?

. . . nyumbani;
Kwa upole, upendo, Yesu anaita,
Anakuita . . .

Njoo nyumbani, njoo nyumbani, (Ee Mungu)
Mlio wachovu, njoni.

219 Je! ishara hizi zinakupa wasiwasi, duniani siku hizi, kuzijua? Ama, hivi mmepita mahali hapo? Kungali kuna mahali mwororo patulivu mle ndani? Kama pako, njoo. Acha aingie ndani, achukue mamlaka, papo hapo. Atakufanya kiumbe kipya. Utaondoka hapa mtu mwenye furaha sana ambavyo hujawahi kuwa.

Anakuita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani.

220 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, hebu tuuvumishe. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, *Kwa Upole Na Upendo*—Mh.] Hivi hutakuja nyumbani hapa? Mungu akubariki, maskini msichana, nimeuona.

Ninyi mliochoka, njoni nyumbani.

Ee uliyerudi nyuma, njoo nyumbani.

Kwa upole, upendo . . .

221 Hivi unahusika? Kama umeshawishika, basi unahusika. Ama, kama hujashawishika bado kwamba ni Yesu, basi huwezi kuhusika.

Njoo nyumbani.

222 Sasa, papa hapa, hadharani, hatuwezi kufanya mengi sana kulihusu, mkisimama hapa. Mmekuja, kukiri.

223 Wakati fulani uliopita, nilisikia hadithi ndogo. Ninawatakeni msikilize, kwa makini. Kulikuwako na mtu jina lake Danny Martin. Alivuka taifa hapa, miamsho mingi mikuu. Wanadai ya kwamba aliota ndoto, usiku mmoja, kwamba alikuwa amekufa. Naye—naye akaanza kwenda Mbinguni; akalakiwa langoni. Akasema, "Ni nani ajaye huku?"

224 Naye akasema, "Huyu ni Danny Martin." Akasema, "Mimi ni mwinjilisti."

225 Yule mtu langoni, kasema, "Hebu tuone kama jina lake liko hapa kwenye kitabu." Kasema, "Halipo."

Akasema, "Vema, nilikuwa mhudumu."

226 Kasema, "Sijali ulikuwa nani. Kama jina lako halimo humu, huwezi kuingia lango hili. Limefungwa na kukazwa! . . . huna budi kuja. Huna budi kuandikwa jina lako kwenye kitabu hiki."

Naye akasema, "Vema, nifanye nini?"

227 Akasema, "Waweza kukata rufaa ya kesi yako, ukitaka, kwenye Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi cha Mungu." Loo, ndugu, dada, kamwe usitamani kwenda kule.

228 Kwa hiyo akasema, "Nafikiri sina lingine ila kukata rufaa ya kesi yangu."

229 Kwa hiyo, akasema. . . Ilionekana kana kwamba alianza tu kwenda mahali fulani; hakujua alipokuwa. Hii ni ndoto ya mtu huyo. Naye akasema, "Nikaingia kwenye Nuru. Hakuna mahali halisi ilipokuwa ikitokea. Lakini nikaenda polepole, na, baada ya kitambo, nikasimama. Nikasikia Sauti, kasema 'Ni nani anayekikaribia kiti Changu cha haki—haki?'"

230 Akasema, "Mimi, Danny Martin." Kasema, "Mimi ni mwinjilisti kutoka Marekani." Akasema, "Ni—ni—ni—niliokoa nafsi. Nao wasingeniruhusu niingie langoni."

231 Akasema, "Vema. Kama umeikatia kesi yako rufaa kusimama mbele ya mahakama Yangu," Yeye akasema, "basi ninahitaji haki." Akasema, "Ninazo zile amri." Kasema, "Danny Martin, hivi ulipata kusema uongo, maishani mwako?"

232 Akasema, "Nilidhani nimekuwa mtu mwaminifu," lakini, kasema, "Mbele ya Nuru hiyo, nilitambua nilisema mambo fulani ya udanganyifu." Kasema, "Naam, Bwana. Nilisema uongo."

Akasema, "Hivi ulipata kuiba?"

Akasema, "Nilidhani nilikuwa mwaminifu, bali niliona baadhi ya mipango."

233 Basi, ngoja mpaka utakapofika Mbele ya hiyo Nuru. Unafikiri uko sawa sasa, bali ngoja tu mpaka utakapofika kule. Hebu jaribu kukaribia wakati mmoja ukiwa umekata nywele, unavuta sigara. Jaribu tu, wakati mmoja. Mnafikiri ninasema tu hayo. Nitawathibitishia, kutoka kwenye Maandiko hapa. Kweli kabisa. Jaribu kuvaa jozi ya suruali fupi, kaptura, uone mahali ulipo. Biblia inasema, "Ni chukizo machoni pa Mungu." Mnaona? Jaribu, wakati mmoja. Dhamira yako iko wapi?

Kasema, "Vema, ulipata kufanya *hili* ama *lile*?"

"Naam," akasema.

"Basi, Danny, ulipata kutenda dhambi?"

Akasema, "Naam, nilitenda dhambi."

234 Naye alikuwa tu karibu kusikia. . . Alisema mifupa yake, ilionekana kama, inatengana; kusikia hilo, "Ondoka uingie katika kuzimu ya milele, kutoka Mbele Zangu."

235 Kasema alisikia sauti tamu sana aliyopata kusikia. Kasema aliangalia kote, kuiona. Kasema aliona uso wa kupendeza kuliko zote alizowahi kuona.

236 Kasema, Yeye alisema, "Baba, hiyo ni kweli. Danny alijaribu kuishi kila kitu alichojua kuishi, lakini kweli alifanya makosa. Lakini jambo moja alilofanya huko duniani, Yeye alinitetea. Alinitetea Mimi, akanisimamia, katika Neno Langu lote. Sasa nitamtetea Hapa."

237 Hilo ndilo unalofanya sasa. Unachukua msimamo kwa ajili Yake hapa. Yeye atakutetea, mbele za Baba.

238 Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utakuwa na rehema na kutoa msamaha wa dhambi za watu hawa. Wamekuja hapa kufanya msimamo. Kila mmoja wao anataka kujazwa na Roho Mtakatifu. Jalia watapewa. Ninawadai, Bwana, kwa ajili ya utukufu Wako, wanaposimama mbele ya wasikilizaji hawa, kama shahidi.

239 Baadhi yao ni wafuasi wa kanisa, baadhi yao wamerudi nyuma, baadhi yao hawajawahi kukukubali hapo kabla. Nao wamesimama hapa. Nao wanaona uchafu unaofuata maungamo halisi, ya kweli ya Mkristo. Nao wako tayari sasa kuchukua msimamo wao, kama yule mwanamke, kukiri kwamba wao ni wenye dhambi. Lakini kwa machozi yao ya toba wanataka kuosha uchafu kutoka kwa Jina Lako, Bwana. Wajalie kwamba wanaweza kufanya hivyo.

240 Sasa nitawaomba jambo moja. Ambapo hamtakuwa hapa nje mbele ya umma, wana chumba kilichotolewa mumu humu nyuma. Kama mkitaka kupokea sasa, nawatakeni mrudi nyuma, kabla hatujaenda kule nyuma pamoja nanyi. Njoni moja kwa moja kwenye vipandio namna *hii*, na mtokee hapa nje. Mtafanya hivyo kwa ajili yangu sasa? Pitieni moja kwa moja *hapa*. Tuna mahali palipoandaliwa hapa kwa ajili yako, rafiki. Njoo moja kwa moja *huku*. Mungu awabariki, kila mmoja.

241 Je! kuna wengine zaidi wangetaka kuja sasa hivi, wakati wakienda? Nataka kila mtu aliye hapa ndani, atoke na kuenda nyuma. Watakutana nanyi katika dakika moja tu. Usiku huu umetolewa kwa ajili ya jambo hili. Huu ndio wakati, mpokee Roho Mtakatifu. Hujawahi kumpokea kamwe; huu ndio wakati. Njoo sasa na umpokee. Huu ndio wakati wa kujiweka sawa na Mungu. Ungali unaweza kufanya uamuzi wako. Sasa, kama hutafanya hivyo, Yeye hatakutetea Kule! . . .? . . .

242 Bwana abariki. Inaonekana kama, kila mmoja wao anaenda. Ninaamini wao ni waaminifu kabisa. Ninaamini huu utakuwa ndio usiku mkuu kuliko wowote tuliowahi kuona huku Tampa kwa muda mrefu. Hivi mtu mwingine atakuja hapa mbele sasa? Hawa ni wafanya kazi mahususi pale nyuma, walio na vitambulisho vyao, wakiingia pamoja nao. Tunaingia mle, katika dakika chache tu, kuwa moja kwa moja pamoja nao kule. Wangali watakuwa ndani ya jengo. Ninyi ndugu ingieni mle mkakutane nao basi, hima, watenganisheni chumbani. Nitakuwa mumo humo pamoja nanyi, katika dakika moja tu.

243 Hivi mtu mwingine si aje upesi sana, wakati wakienda sasa? Simama tu moja kwa moja.

244 Ungemwacha Yesu aketi leo hii? Unasema, “Kama ningalikuwa huko nyuma, kama ningalimwona namna hiyo, nisingefanya hivyo.” Na sasa hivi je? Msimamo wako mwenyewe

wa sasa unatambulisha kile ungefanya wakati huo. Unaona? Msimamo unaochukua sasa, unajisikia kwamba wewe ni mzima kutosha? Vema. Hiyo ni kati yako na Mungu. Mimi si hakimu. Mimi ninawajibika tu kwa Neno. Mnaona? Yeye yupo hapa katika mikutano hii. Wanakuja kutoka makanisani, pia, bali wanaenda kulitatua sasa hivi. Ni hayo tu. Wako tayari. Kwa nini unataka kuishi maisha ya Mkristo nusu-nusu? Ama umtetee Mungu, au umpinge, kusudi ulimwengu ujue jinsi ulivyo na mahali unaposimama.

245 Mungu awabariki wakati wakienda. Wanaingia, kama tu, wapate kufa kwa nafsi zao. Wanaenda kuyatoa maisha yao. Wanaelekea Kalvari. Watasulubiwa kwa ajili ya mambo ya ulimwengu, na mitindo ya siku hii yenye madoido tunayoishi hapa. Wanaenda kumfia Yesu Kristo, ambaye Uwepo Wake upo hapa sasa hivi. Wanaenda wapate kufa kwa nafsi zao, wakazaliwe upya kwa Yesu Kristo. Mungu awabariki.

Kuna mtu mwingine atakayekuja, tunapoimba polepole sasa?

> Kwa upole, upendo, Yesu anaita,
> Anakuita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani.
>
> Njoo nyumbani,

Utafanya hivyo?

> Njoo nyumbani,
> Enyi mliochoka, njoni nyumbani.

246 Sasa, kwa upole, Roho Mtakatifu anaonekana tu kuwa moyoni mwangu, akilia tu. Ninajua kuna wengi sana wasio naye.

> Anakuita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani.

247 Kutoka kwenye roshani, kutoka kila mahali, kumbukeni, ninawapa Yesu Kristo. Je! mtampokea? Mtampokea? Utampokea, dada yangu? Utampokea, ndugu yangu? Njoo ukafanye ninii yako . . . ukafanye upya nadhiri yako usiku wa leo na ufanye ahadi kwamba utamtumikia.

248 Nanyi mnajua nisingekuwa nimesimama hapa, nikisema hivyo, kama sikuwa chini ya utambuzi. Mtu fulani anapata wito wao wa mwisho. Sasa, ni aibu kuwavuta watu, ambao hawajampokea. Tunatambua hilo. Lakini ni—ni aibu, kuliona hivi, bali ninakisia haina budi kuwa hivyo. Ndani yangu, kitu fulani tu kinanirarua. Sasa hebu . . .

249 Hebu tu niwaonyeshe baadhi yake. Angalieni hapa, kuwaonyesha tu Yeye angali hapa. Watu walio wagonjwa na wahitaji.

250 Ninamwangalia mtu hapa moja kwa moja ambaye amepoteza hisi yake ya kunusa, ameketi papa hapa, mwanamke. Yeye anaiombea sasa hivi. Kama hiyo ni kweli, mama, inua mkono wako kama hiyo ni kweli.

251 Huyu hapa bikizee, ameketi papa hapa mwishoni. Ndio kwanza aingie humu nchini leo hii. Ametoka Georgia. Ana kivimbe kikubwa mno ndani yake. Yuko hali mbaya sana. Ataamini, anaweza kuponywa. Ndiyo kwanza aje. Nalo jina lake ni Bibi Turner. Utaamini kwa moyo wako wote sasa, Yesu Kristo atakupa afya. Unaamini?

252 Unamwamini Mungu? Wewe ni mgeni? Huna kadi ya maombi, sivyo? Ndio kwanza uje leo. Mtu fulani alikuja na kukuchukua. Umeshuka kuja huku kutoka kwenye mkoa wa Georgia. Je! unaamini sasa ya kwamba—ya kwamba Mungu . . . Mwanao alikuja akakuchukua. Vema. Sasa, unajua haiwezekani kabisa kwangu kujua hilo, maana umekuja muda mfupi tu uliopita, na ukaketi chini hapa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mnaona?

253 Sasa, Roho Mtakatifu yeye yule anayesema hayo, anasukuma dhidi ya watu papa hapa. Mnaona? Yeye ametambulishwa, jamani. Msininii, msifanye hivyo. Msifanye. Una—unafanya kosa la kijinga. Ninawapenda. Kumbukeni, mmekuja kunisikiliza. Ninathamini hilo. Upendo husahihisha.

254 Ukimwona mtoto wako hapa mtaani, utasema, useme tu, “Kadogoo, hupaswi kufanya hivyo?” Utaondoka, na kumfanya akae ndani, kama unampenda.

255 Upendo husahihisha, sio kukupapasa. Sina budi kuwakemea. Kumbukeni, hata ni sadaka zenu na kadhalika, zinazolipia mkutano huu, na zinafanya iwezekane kuwapo hapa. Hivi ninawapenda? Kwa moyo wangu wote.

256 Dada, huenda ukafikiri sasa nina jambo fulani dhidi yako, kwa kufanya mambo haya ufanyayo. Si kwamba nina chochote dhidi yako, dada. Ni upendo wangu wa kiungu kwako.

257 Mtu fulani alisema, “Kama ungalikuwa mdogo kidogo, usingewazia hilo.” Niliwazia haya nilipokuwa na umri wa miaka kumi na minne. Biblia inasema hivyo. Ni jambo lile lile.

258 Usifanye kosa hilo. Usitumainie kunena kwa lugha kwamba ni Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hunena kwa lugha, bali usitumainie hilo na kufanya mambo unayofanya, kucheza katika Roho, namna fulani ya mhemko. Kristo ni Mtu. Hakika. Wakati . . . Naye ni Neno. Na kama yumo mle ndani, Yeye daima hulifanya Neno Lake litende kazi kama tu vile linavyopaswa. Unapolikataa, inawezaje kuwa ni Kristo?

Njoo nyumbani, njoo.

259 Mlango ungali umefunguliwa. Kumbukeni, kwenye ile Hukumu, mimi sina hatia.

Enyi mliochoka . . .

260 Yesu Kristo akijitambulisha miongoni mwenu, akithibitisha hilo, Roho yuyo huyo. Yeye alisema, “Katika siku atakapofunuliwa Mwana wa Adamu.” Ni yeye yule jana,

leo, Yesu yeye yule aliyeketi na miguu michafu. Angeunga mkono mnafiki? Angemuunga mkono mtu ambaye hakufahamu Neno Lake? Huo ni utambulisho ya kwamba anajua Neno. Ninawaambia Kweli. Msilipite.

Njoo nyumbani.

261 Mara ya nwisho. Akisimama hapa, tayari kukutana nanyi. Nafasi, kuna nafasi kubwa mle. Watu wamepiga magoti, kila mahali.

Enyi mliochoka, njoni nyumbani.

Mungu uturehemu, uturehemu. Huwezi kusikia kuugua huko sasa?

Kwa upole, upendo, Yesu anaita;
Anakuita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani.

Njoo nyumbani, njoo nyumbani.

Mungu akubariki, ewe kijana mwanamume. Msimamo adhimu.

. . . njoo nyumbani;
Kwa upole, upendo, Yesu anaita;
Anakuita, Ee mwenye dha-. . .

262 Mwenye dhambi ni nini? Si hao wanaovuta sigara. Kuvuta sigara si dhambi. Kunywa pombe si dhambi. Kulaani si dhambi. Kufanya uzinzi si dhambi. La, la. Hizo ni sifa za kutokuamini. Unafanya hayo kwa kuwa wewe si mwaminio.

263 Kuna mawili tu: moja, wewe ni mwaminio, ama si mwaminio. Kama wewe si mwaminio, haidhuru wewe ni wa kidini jinsi gani, ungali ni mwenye dhambi. Ungali ni mwenye dhambi, kama hukubali kila Neno la Biblia hiyo, kila Neno Lake. "Kwa kuwa mbingu na nchi zitapita, bali si hata yodi moja wala nukta itapita kutoka kwenye Hilo." Nasi tutatoa hesabu kwa ajili yake.

264 Unasema, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa. Watu wangu hawaninii . . ." Hilo halijalishi. "Ninafanya *hivi*." Sijali yale umefanya.

265 Wewe ama ni mwaminio au mwenye dhambi. Hilo ni kali kweli. Lakini ninasema tu jambo hili, kwa sababu, Yeye yule anayeijua mioyo yenu ananiambia niliseme.

266 Mmemaliza? Ninawaona wawili zaidi wakija. Ninangoja tu, maana sijui kama huenda kukawa na mtu mwingine, mwanamke mmoja tu. Mbona usije, uingie wakati maji yametibuliwa sasa? Litakuwa ni jambo kubwa, katika dakika chache tu, hapa nyuma. Njoo, sivyo? Inuka kutoka hapo.

267 Fanya nadhiri yako kwa Mungu, "Bwana Mungu, nisamehe kwa yale ambayo nimefanya. Ninakuahidi. Nilisema nilikuwa Mkristo. Lakini, Bwana, kuna Kitu fulani ndani yangu, kinachoniambia ni—ni—nimehukumiwa sasa hivi Mbele ya Huyu anayejitambulisha kama Bwana Yesu Kristo. Nimehukumiwa,

moja kwa moja moyoni mwangu. Na nikijua ya kwamba, hapa ndani, nikilifanya hili dhahiri sana, nimehukumiwa. Ninaingia, kulifanya hili sawa, sasa hivi. Nitamwahidi Mungu, papa hapa, kwamba, tangu usiku wa leo na kuendelea, kabisa nitamwishia." Hivi huwezi kufanya hivyo? Vema.

268 Wakati, kama ni hao tu, sasa hebu tusimame, ninyi huko nje, kwa dakika moja tu. Laiti ningaliweza kuimba. Ningependa kuimba wimbo huo.

> Nisamehe, Bwana, na unijaribu mara nyingine tena.
> Nitakuwa Wako, Bwana mpendwa, kama utakuwa wangu.
> Kama nikianguka, ama kama nikishindwa, jalia nisimame na kujaribu tena.
> Nisamehe, Bwana. Nijaribu mara nyingine tena.

269 Ni wangapi hapa sasa walio Wakristo, na mnaamini ya kwamba mmetiwa nanga katika Kristo, nanyi mko tayari kwa ajili ya Hukumu ijayo? Nanyi mtaweza, kwamba, parapanda itakapolia, hakutakuwako na jambo moja la kufanya ila kunyakuliwa? Itafanyika upesi sana, hutakuwa na wakati wa kufanya jambo lingine, "Katika dakika moja, kufumba na kufumbua." Itakuwa nini, moja ya siku hizi? Vipi kama uliukosa pale, daima, Milele, daima, milele, milele? Wakati huu mdogo wa anasa za dunia utamaanisha nini? Bure.

270 Sasa, nafikiri sisi sote tunapaswa kuyaweka wakfu maisha yetu, hapa nje, kwa Kristo. Sivyo? Ni wangapi wangetaka kuyaweka wakfu maisha yenu upya juu ya hili, usiku wa leo? Nitajiweka wakfu tena, sasa hivi. Bwana. . .Sasa wazia kile ninii. . .kwamba dhambi yako ikuzingayo ni nini, na hebu tuinue tu mikono yetu sasa kwa Mungu, kila mmoja, kwa njia yenu wenyewe.

271 Kumbukeni, Yeye yupo kila mahali. Wakati kukiwako na labda elfu moja mia nane ama elfu mbili wakiombea humu ndani, kuna mamilioni wanaoomba kote ulimwenguni wakati huo huo, na Yeye anamsikia kila mmoja wao. Hakuna hata shorewanda anayeweza kuanguka barabarani, pasipo Yeye kujua. Anajua kila siri ya moyo wako.

272 Hebu tuombeni sasa kwa njia yenu wenyewe, tujiweke tu wakfu kwa Kristo.

273 Bwana Yesu, mimi. . .Uwepo Wako ulikuwa mkuu sana, dakika chache tu zilizopita, hata ilikuwa ni vigumu mimi kuzuia pumzi yangu. Ilionekana kana kwamba ningeaga. Nami ninajua kuna sababu ya Wewe kutaka hili lifanywe jinsi hii. Si—sielewi, bali Wewe unaelewa, Bwana. Wewe ni Mungu. Lakini umejitambulisha Mwenyewe dhahiri. Upo hapa. Tunakuamini. Tunajua Wewe upo hapa.

274 Na humu jengoni, kuna mamia ya mikono iliyoinuliwa. Tunajiweka wakfu upya.

275 Bwana, juu ya mimbara hii ambamo nimehubiria, na kukuona Wewe umesimama hapa ukijitambulisha juma hili, na—na—najiweka wakfu upya. Najiweka wakfu upya kwa huduma Yako. Nisamehe manung'uniko yangu yote kuhusu kuchoka. Na—na—na, Mungu, nichukue tu mikononi Mwako.

276 Tuchukue sisi sote, Bwana. Tuondolee mbali kutoka kwa shughuli hizi za ulimwengu, na mambo haya ya kilimwengu, Bwana, tupate kuwa watumishi waliotengwa, waliowekwa wakfu, wa Bwana Yesu Kristo. Tujalie, Baba. Tusikie usiku wa leo.

277 Wabariki hao walio huko nyuma, wanaoutafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Jalia sauti itoke Mbinguni tena, kama upepo mkali, ukienda kasi. Jalia ijaze kila mtu humo ndani, na Moto kutoka kwenye madhabahu ya Mungu. Tujalie, Bwana.

278 Tunakusifu. Tunakupa shukrani na sifa kwa—kwa kutupokea. Tunakupa shukrani na sifa kwa ajili ya watu Wako. Tunakusifu kwa sababu Wewe ulisema, "Kama tutaungama dhambi zetu, Mungu ni wa haki kuzisamehe." Tujalie, Bwana, sote tupate kusamehewa. Ndipo kesho tutaona mkutano mkubwa kuliko yote ya uponyaji nchi hii iliyopata kuona, kwa sababu ya maungamo yetu. Tujalie, Bwana. Tunajiweka wakfu Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Njoo, Ndugu Cox.

279 Jiwekeni tu wakfu kwa Mungu, kila sehemu mle ndani. Nitamwomba Ndugu Cox sasa, mmoja wa wachungaji wenu hapa, aendeleze maombi.

Yesu Hutimiza Miadi Yake Yote SWA64-0418E
(Jesus Keeps All His Appointments)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 18 Aprili, 1964, kwenye Ukumbi wa McKay huko Tampa, Florida, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha Ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na umechapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org